SUPA JACKPOT
TZS. 1,029,401,974
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**MADIWANI** waingia matatani kwa kutafuna fedha za halmashauri




UKURASA 11

Nipashe
Jumamosi Septemba 10, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581064
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Kilio cha tozo chazidi kuvuma

**TUCTA**, TALGWU zataka zifutwe, zalia nyongeza kidogo ya mishahara...*Endelea ukurasa 2*



Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya

Mkuu wa Idara ya Habari na Uhusiano wa Kimataifa wa TALGWU, Shani Kibwasali.

## Samia: Malkia Elizabeth II atakumbukwa kwa hili

UKURASA 4 & 17





Rais Samia Suluhu Hassan akitia saini kitabu cha maombolezo kufuatia kifo cha Malkia Elizabeth II wa Uingereza katika makazi ya balozi wa nchi hiyo, Oysterbay jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 3

### MBARONI MADAI KUMUUA MTOTO KISHA KUMFUKIA

Jeshi la Polisi Mkoani Njombe, linamshikilia Happiness Mkolwe (27) kwa tuhuma za mauaji ya mtoto Jackson Kiungo (6), mwanafunzi wa darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Ihanga na kujaribu kumfukia katika shimo alilolichimba...

UKURASA WA 17

### MWILI MALKIA ELIZABETH II UTAKAVYOAGWA, KUZIKWA

DUNIA iko katika maombolezo baada ya Malkia Elizabeth II wa Uingereza kufariki dunia siku ya Alhamisi...

## Daktari kizimbani shtaka la ubakaji

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA, YANGA MGUU SAWA AFRIKA UK.24

**KABWELA** UK. 18

# TUCTA nao watia neno sakata tozo

**Na Mary Geofrey**

SHIRIKISHO la Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) limeungana na wadau wengine kupinga tozo za miamala ya kielektroniki iliyoanza kutekelezwa mwaka mpya wa fedha.

Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya, jana aliweka wazi msimamo wa shirikisho hilo ni kufutwa kwa tozo hizo, huku akiunga mkono hatua zilizochukuliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) chini ya Mwenyekiti wake, Rais Samia Suluhu Hassan. Nyamhokya, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema wafanyakazi ni wahusika wakubwa wa tozo hizo ambao wanalipa kodi (PAYE) na kukatwa tena fedha zao wanapozichukua benki.

"Tangu kuanza kwa mwaka wa fedha, ilipitishwa sheria inayohusiana na masuala ya tozo na imeleta shida hasa kwa wafanyakazi kwa kuzingatia wanapitisha mishahara yao kwenye benki mbalimbali nchini," alisema Nyamhokya.

"Tumepokea taarifa nyingine baada ya kikao cha Kamati Kuu ya CCM kilichofanyika Septemba 7 kuwa imeishauri serikali kukaa kujadili upya tozo hizi, baada ya kuona chama kinachoongozwa na Rais Samia kimeona umuhimu na kusikia kilio cha wadau na kutoa msimamo huu, tusikae kimya tutoe kauli yetu," alisema.

Nyamhokya alisema awali waliwasilisha mapendekezo yao serikalini kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), George Simbachawene, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako na Naibu Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi. Alisema ombi lao kubwa ni kufutwa kwa tozo hizo na serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kufikiria njia mbadala za kupata tozo.

"Serikali iziondoe kabisa kwa sababu wafanyakazi wanalipa PAYE, wataalamu wetu kutoka sekta mbalimbali wapo tayari kushirikiana na serikali kutoa maoni yao maeneo ambako zinaweza kukatwa tozo hizo," alisema Nyamhokya.

Mkuu wa Idara ya Habari na Uhusiano wa Kimataifa wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU), Shani Kibwasali, alisema tozo hizo ni mzigo mkubwa kwa wafanyakazi.

"Ili kupunguza kadhia hii kwa wanachama wetu, tunaiomba serikali kufanya mabadiliko ya sheria ya tozo za miamala ya benki ili kuepuka malipo mara mbili katika mshahara mmoja wa mtumishi wa umma.

"Hii inazidi kumbebesha mzigo na kumkandamiza mfanyakazi hasa kwa kuzingatia mishahara wanayopata haikidhi mahitaji yao ya kila siku na familia zao," alisema Kibwasali.

Juzi Kamati Kuu ya CCM ilielekeza serikali kutazama na kuchukua hatua kuhusu tozo za miamala ya kielektroniki iliyoanza kutekelezwa hivi karibuni.

Katibu wa NEC Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alieleza hatua ambazo chama hicho kimetaka zichukuliwe kuwa ni kuzingatia maoni na ushauri wa wananchi.



Rais mstaafu Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuhojiwa na kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa, jijini Dar es Salaam jana. Kulia kwake ni Mwenyekiti wa Kikosi hicho, Prof. Rwekaza Mukandara. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Daktari kortini madai ya kubaka na kulawiti

**Na Grace Gurisha**

DAKTARI wa Hospitali ya Rufani ya Amana, Joseph Mwaipola (50), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa madai ya kubaka na kumlawiti binti wa miaka 17.

Akisoma hati ya mashitaka, Wakili wa Serikali Silvia Mitanto, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Yusto Ruboroga, kuwa daktari huyo anashtakiwa kwa mashtaka matatu.

Mitanto alidai katika shtaka la kwanza, Mwaipola ambaye ni Mkazi wa Mtoni Kijichi, katika tarehe zisizofahamika Februari, mwaka huu, akiwa eneo la Hospitali ya Rufani ya Amana ndani ya Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, alimbaka binti wa miaka 17 (jina limehifadhiwa).

Katika shtaka la pili, mshtakiwa anadaiwa Mei 31, 2022 akiwa katika nyumba ya kulala wageni ya Panzuri iliyoko Temeke, Dar es Salaam alimbaka binti huyo.

Inadaiwa kuwa, kati ya Februari, 2022 mshitakiwa akiwa eneo la Hospitali ya Amana ndani ya Wilaya ya Ilala, alimlawiti binti mmoja mwenye miaka 17 (jina limehifadhiwa).

Baada ya mshtakiwa kusomewa mashitaka yake, alikana kuhusika na tuhuma hizo na Wakili Mintanto, alidai upelelezi wa shauri hilo umekamilika na pia hawana pingamizi la dhamana kwa sababu mashtaka yanayomkabili yanadhaminika.

Pia, aliomba mahakama itoe masharti ya dhamana ambayo yatamfanya mshtakiwa awe anahudhuria mahakamani. Hakimu Ruboroga, alisema ili mshtakiwa awe nje kwa dhamana, atatakiwa awe na wadhamini wawili wa kuaminika.

Alisema, wadhamani hao wanatakiwa wawe na barua za utambulisho na kitambulisho cha taifa au cha kupigia kura na wadhamini hao pamoja na mshitakiwa watatia saini bondi ya Sh. milioni tano kwa kila mmoja.

Mshtakiwa alitimiza masharti hayo na kuachiwa kwa dhamana hadi Oktoba 5, 2022 atakaposomewa maelezo ya awali.

# ...TALGWU walia na nyongeza mishahara

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) kimesema hakijaridhishwa na nyongeza ya mishahara iliyofanyika.

Mei 14 mwaka huu Rais Samia Suluhu Hassan alitangaza nyongeza ya mishahara ya watumishi wa umma kwa asilimia 23.3.

Mwaka wa fedha wa 2022/23 unaoendelea, nyongeza hiyo mpya ya mishahara imeanza kutolewa kwa watumishi wa umma, huku kukiwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wadau kwamba ongezeko hilo ni dogo.

Mkuu wa Idara ya Habari na Uhusiano wa Kimataifa TALGWU, Shani Kibwasali, alibainisha msimamo wa chama hicho jana alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu taarifa ya utekelezaji wa shughuli za chama kwa kipindi cha miezi sita.

"Labda niseme, ni ukweli usiofichika kwamba wanachama wetu ambao ni waathirika wakubwa katika suala hili, bado wana manung'uniko na TALGWU kama msemaji wao, hatujaridhika kabisa kwa jinsi nyongeza ya mishahara ilivyofanyika.

"Ila ninaomba niwatoe hofu wanachama wetu kwamba suala hili linashughulikiwa na chama kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA)," alisema Kibwasali.

Julai 29 mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumzia suala la nyongeza ya mishahara, alisema asilimia 23 ya nyongeza ya mishahara iliyotamkwa, iliwalenga watumishi waliokuwa wanalipwa kima cha chini ambao ni kati ya asilimia 75 hadi 78 ya wafanyakazi wote.

Pia alisema kuwa katika kipindi cha miezi sita ya mwaka huu, TALGWU imefanikiwa kushughulikia kesi 140 za wafanyakazi. Kati yake, 39 zimeshughulikiwa huku 35 walishinda nne walishindwa.

Alisema kushinda kwa kesi hizo ni ushahidi kwamba wanatekeleza jukumu la kuhakikisha haki inatendeka kwa wanachama wao katika hatua za awali wakati mtuhumiwa anakamatwa.

"Chama chetu huhakikisha mwanachama anapata haki ya kuwasiliana na viongozi wa chama au wakili wa chama, kuwapo ndugu, jamaa, rafiki au wakili pindi anapoanza kuandika maelezo, ili yatumike kama ushahidi na upande wa Jamhuri," alisema Kibwasali.

## Mbaroni madai kumuua mtoto kisha kumfukia

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

Jeshi la Polisi Mkoani Njombe, linamshikilia Happiness Mkolwe (27) kwa tuhuma za mauaji ya mtoto Jackson Kiungo (6), mwanafunzi wa darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Ihanga na kujaribu kumfukia katika shimo alilolichimba.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa.

Kamanda Issah, alisema siku ya tukio mwanafunzi huyo alikwenda saluni kunyoa lakini katika hali ambayo si ya kawaida, Mkolwe huyo alimfuata na baada ya kumaliza kunyolewa, alimchukua na kuondoka naye kwenda alikojua mwenyewe.

Alisema alipofika huko, alimsababishia kifo na kumvua nguo kisha kumfukia na baadaye kumfunika na mabanzi ambayo yalikuwapo katika eneo hilo.

Issah alisema, mwanamke huyo baada ya kufanya tukio, aliamua kuchimba kaburi ili amfukie.

"Lakini macho kuona walimwona mama huyo, hivyo hakuendelea na tukio hilo la kumfukia ingawa tayari alikuwa ameazima vifaa kwa ajili ya kutenda jambo hilo. Baada ya kufuatilia, tumeona vitu vya namna hiyo," alisema Issah.

Kamanda Issah alisema jambo la kushangaza, ni kuwa mwanamke huyo alipoulizwa alikataa katakata lakini baadaye alionyesha mpaka nguo ambazo mwanafunzi huyo alivaa kabla ya kukutwa na umauti.

Alisema kisa kilichosababisha mauaji hayo, kwa mujibu wa maelezo ya mwanamke huyo, ni kwamba wametengana na mumewe na kuna mwanamke mwingine ambaye ni mama wa mwanafunzi huyo alikuwa anakunywa pombe na mumewe, hivyo alipopewa taarifa hiyo na watu wake, aliamua kulipiza kisasi.

Issa alisema, mwanamke huyo alikamatwa juzi baada ya jeshi hilo kupata taarifa kuwa Septemba 6, mwaka huu, kuna mwanafunzi amepotea.

Alisema, ukatili dhidi ya watoto kwenye baadhi ya maeneo mkoani Njombe upo ndiyo maana mkoa huo umeelezwa kuwa ni moja ya maeneo yaliyokithiri matukio hayo.

"Ndiyo maana walikuwa wanasema watoto wameuawa na watu wasiojulikana kitu ambacho si kweli bali ni mambo ya kifamilia na mtu wa karibu wanayafanya mauaji hayo," alisema Issah.

Alisema, matukio yanayohusisha mauaji ya watoto wengi wao ni umri wa miaka sita kwani akivuka umri huo inakuwa bahati kwa mtoto huyo.

# RC ataka madiwani kurejesha fedha walizotumia kinyemela

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ametoa siku tano kwa madiwani katika halmashauri zote za mkoa huo waliotumia fedha za halmashauri kinyume cha utaratibu kuzirejesha haraka.

Serikamba, alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ikiwa ni mwendelezo wake wa kutembelea halmashauri zote na kuzungumza na madiwani kama sehemu ya kujitambulisha.

Hatua ya mkuu wa mkoa kutoa agizo hilo, inatokana na kuwapo taarifa kwamba baadhi ya madiwani walikusanya fedha kwenye vizuizi vya mazao (mageti) lakini hawakuzipeleka benki na badala yake walizitumia kinyume cha utaratibu.

Serukamba, aliwagiza wakurugenzi wa halmashauri zote kuhakikisha wanaunda kamati ndogo ambazo zitakuwa zikikutana kwa wiki mara mbili katika kila halmashauri ili kutathimini mapato ya kila chanzo cha fedha.

Alisema, kuundwa kwa kamati hizo, kutasaidia kushughulikia upotevu wa mapato katika kila halmashauri na kwamba suala hilo litakuwa la kufa na kupona.

Pia, alionya tabia ya baadhi ya watendaji ambao wengi wao wanakusanya hela katika vyanzo mbalimbali vya fedha pasipo kuzipeleka benki jambo ambalo limekuwa likisababisha upotevu wa fedha za halmashauri.

Serukamba alisema, kiwango cha makusanyo katika kipindi cha robo mwaka kwa baadhi ya halmashauri za mkoa wa Singida hakiridhishi, hivyo ni jukumu la kila mkurungezi wa halmashauri kupitia upya vyanzo vyake vya mapato na kuhakikisha fedha hazipotei.

Alisema, watendaji wa kata na vijiji wahakikishe wanawahimiza wakulima kuanza kuandaa mashamba yao kwa wakati kwa kuwa mkakati wa mkoa kwa mwaka huu ni kuongeza uzalishaji wa mazao ya alizeti, mahindi, mpunga,mbaazi na viazi.

Kwa mujibu wa Serukamba, mkoa umejipanga kuongeza uzalishaji wa alizeti kwa kuongeza maeneo ya kulima ili kulifanya taifa lijitosheleze kwa mafuta ya kula. Alisema serikali imeboresha mazingira ya kilimo kwa kupunguza bei ya mbolea na ruzuku katika mbegu bora za kilimo.



Balozi wa Indonesia nchini, Tri Yogo Jatmiko (kushoto), akizungumza na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omary Mgumba (wa tatu kulia), alipotembelea mkoani humo jana, kwa lengo la kutaka kufanya uwekezaji wa mazao ya viungo ikiwemo nazi na karafuu. Wa (pili kulia) ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga, Pili Mnyema. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

## TRA yaendelea kumkaba koo mfanyabiashara kodi ya gari

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imesema mfanyabishara maarufu wa Zanzibar, Toufiq Salum Turky, bado hajalipa Sh. milioni 308.5 za kodi kutokana na kuingiza gari la kifahari aina ya Benzi, Januari, mwaka huu.

Naibu Kamishina wa TRA Zanzibar, Juma Bakary Hassan, aliwaambia waandishi wa habari jana ofisini kwake, Kinazini, Unguja kuwa gari hilo ilingizwa na mfanyabishara huyo kupitia kampuni yake ya Mifuko Turky ya Zanzibar.

Juma alisema, kiwango hicho cha kodi kinatakiwa kulipwa baada ya maombi ya masamaha wa kodi kukataliwa mara mbili na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum.

"Baada ya maombi ya msamaha wa kodi kukataliwa mara mbili na kutakiwa alipe, waliomba kufanyike tathmini upya baada ya kutia shaka kiwango walichokuwa wanatakiwa kulipa kwamba ni kikubwa lakini hesabu ilikuja ile ile ya mwanzo kulingana na thamani ya gari," alisema Juma.

Alisema, baada ya kutakiwa alipe, aliomba wapewe muda wa kulipa kidogo kidogo kwa madai hali ya kifedha si nzuri na kulazimika kupewa miezi mitatu kuanzia Mei hadi Agosti, mwaka huu.

"Mpaka muda unamalizika Agosti, amelipa Sh. milioni 138 na bado wanadaiwa Sh. milioni 170 kati ya Sh. milioni 308 .5 alizopaswa kulipa. Tunajiandaa kuhakikisha fedha hizo zinalipwa kupitia bodi ya dhamana aliyokuwa ameweka kwa kutumia taasisi moja ya fedha," alisema.

Barua mbili za maombi ya msamaha wa kodi zilizotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa wa Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Sheriff Ali Sharif, ziliweka wazi kwamba, mdaiwa anapaswa kunufaika na msamaha wa kodi kupitia Kampuni ya Mifuko Turky kama mwekezaji.

Hata hivyo, maombi hayo yalikataliwa na Waziri Mkuya kwa sababu muda wa kunufaika kisheria ulikuwa umemalizika baada ya ujenzi wa kiwanda cha mifuko kuwa umekamilika na uzalishaji kuanza muda mrefu.

"Unaweza kunufaika na msamaha wa kodi kama mwekezaji wakati wa ujenzi wa mradi na si baada ya ujenzi kukamilika na uzalishaji unaendelea kufanyika," alisema ofisa mmoja mwandamizi wa ZIPA.

Wakati hayo yakiendelea, Bodi ya Mapato Zanzibar ilishasajili gari hilo la kifahari la kutoa namba Z-1 kwa malipo ya Sh. milioni 15, na kuonekana likitembea barabarani kabla ya kukamilisha malipo ya kodi.

"Sisi tumesajili na kutoa namba kwa masharti gari lisitembee mpaka wakamilishe taratibu za kodi tukazo kutoa kibali cha umiliki wa gari," alisema Meneja Uhusiano na Huduma kwa Walipakodi ZRB, Makame Mohammed Khamis.

Gari hilo lenye thamani ya Dola za Marekani 214,668.71, liliingizwa kupitia bandari ya Malindi na kampuni ya uwakala wa mizigo ya Kimataifa HT Motors Group LTD (UK) kwa kushirikiana na kampuni ya uwakala wa mizigo ya ZARA Freight Forwaders ya Malindi, Zanzibar.

# Samia: Malkia Elizabeth II atakumbukwa kwa hili

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema amepokea kwa masikitiko kifo cha Malkia Elizabeth II wa Uingereza na kueleza kuwa atakumbukwa duniani kote kama nguzo ya amani, umoja na utulivu.

Malkia Elizabeth II alitangazwa juzi kufariki dunia akiwa na umri wa miaka 96 na akiwa ameitawala nchi hiyo kwa miaka 70.

Katika ukurasa wake wa Twitter jana, Rais Samia aliandika: "Nimesikitishwa na taarifa za kifo cha Malkia Elizabeth II. Kwa niaba ya Watanzania wote, ninatuma salamu za pole kwa Familia ya Kifalme (Royal Family) na raia wote wa Uingereza.

"Malkia atakumbukwa duniani kote kama nguzo ya amani, umoja na utulivu."

Mbali ya salamu hizo, Mkuu wa Nchi alitia saini kwenye kitabu cha maombolezo katika makazi ya Balozi wa Uingereza nchini yaliyoko Oysterbay jijini Dar es Salaam. Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, jana alituma salamu za rambirambi kwa Familia ya Kifalme na raia wa Uingereza kufuatia kifo hicho.

Taarifa mbalimbali zinazoendelea kutolewa baada ya kifo chake, zilisema Malkia Elizabeth II alifariki dunia kwa amani akiwa amezungukwa na watu wa familia yake katika kasri la Balmoral huko Scotland.

Katika taarifa yake, Mfalme Charles alisema, "Kifo cha mama yangu mpendwa Malkia ni wakati wa huzuni kubwa kwangu na wanafamilia wote.

"Tunaomboleza sana kifo cha Malkia mpendwa na Mama anayependwa sana. Ninajua kumpoteza ni jambo litakalosikika sana kote nchini, Milki na Jumuiya ya Madola na kwa watu wengi duniani kote."

Elizaberth II alizaliwa jijini London Aprili 21, 1926, aliukwaa wadhifa wa Malkia akiwa na umri wa miaka 25, mnamo mwaka 1952 baada cha kifo cha baba yake aliyekuwa mfalme wa taifa hilo, David IV.

Novemba 20,1947, Malkia Elizabeth alifunga ndoa na Mwana Mfalme Philip aliyekuwa Luteni kwenye Jeshi la Wanamaji la Uingereza ambaye alizaliwa katika familia za kifalme za Ugiriki na Denmark.

Alimuoa baada ya kuukana uraia wake wa awali na kuwa raia wa Uingereza.




Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza (kushoto), akitoa elimu kuhusu rushwa ya ngono kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Minazini, Mwananyamala mkoani Dar es Salaam jana, ikiwa ni mwendelezo wa awamu ya tano ya kampeni iitwayo 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana'. **PICHA: SABATO KASIKA**

# 'Wanunuzi wa tumbaku wasiolipa washtakiwe'

**Na Mwandishi Maalum,** KALIUA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza wanunuzi wote ambao wamechukua tumbaku za wakulima na hawajawalipa fedha zao, wachukuliwe hatua za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani kwa kuwa serikali inataka kuona wakulima wakinufaika na zao hilo.

"Tumbaku katika Mkoa wa Tabora ni uchumi, hivyo viongozi kuanzia ngazi ya wizara, mkoa, wilaya, kata na hata vijiji simamieni ushirika kwenye maeneo yenu, ushirika ni uchumi. Sote tuwajibike kwa pamoja, tuhakikishe ushirika unapata mafanikio," Majaliwa aliagiza jana.

Waziri Mkuu alikuwa anazungumza na viongozi wa Vyama Vikuu vya Ushirika (AMCOS) na wakulima wa tumbaku kutoka wilaya za Urambo na Kaliua mkoani Tabora.

Alisema serikali haitasita kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote atakayebainika kuhujumu ushirika nchini kwa sababu imedhamiria kuuboresha.

Aliwaagiza viongozi wa vyama vikuu vya ushirika waende kwa wakulima na kushirikiana nao kutatua matatizo yao. "Kutaneni na viongozi wa mkoa na wilaya na muwaeleze kero zenu, viongozi wa serikali nanyi wapokeeni na muwasikilize," Majaliwa aliagiza.

Waziri Mkuu pia aliwataka viongozi wa serikali kuanzia ngazi ya kijiji, wasimamie mwenendo wa ushirika katika maeneo yao na wahakikishe hakuna migogoro, wizi wala dhuluma kwa wakulima.

"Hatua zichukuliwe kwa watakaowadhulumu wakulima," Waziri aliagiza na kusema kuwa serikali imedhamiria kuendelea kusimamia ushirika wa mazao mbalimbali likiwamo la tumbaku, hivyo akawasisitiza viongozi hao waongeze usimamizi ili kuimarisha maisha ya wakulima wa zao hilo.

Alisema kitendo cha viongozi wa AMCOS kwenda kwa Waziri Mkuu na kuwasilisha kero zao wakati katika maeneo yao kuna viongozi, kinaonesha kuna shida, akiwasisitiza viongozi wa halmashauri watekeleze majukumu yao ipasavyo.

Waziri Mkuu pia alitumia fursa hiyo kuwakumbusha maofisa ushirika nchini watekeleze agizo lake la mwaka jana la kuandaa kanzidata ya wakulima ili kuiwezesha serikali kuwatambua wakulima na kurahisisha utoaji huduma.

Baadhi ya wakulima wa zao la tumbaku waliozungumza kwenye mkutano huo, waliipongeza serikali kwa kuendelea kutoa ruzuku ya mbolea ambayo imewasaidia kuongeza tija katika kilimo.

Pia waliomba uwekwe utaratibu wa kuwahishwa kwa pembejeo za kilimo ili kufikia malengo yao ya uzalishaji na kuwataka maofisa ugani wafike mapema kwa wakulima badala ya kusubiri wakati wa mavuno ndipo watoe kasoro.

## Bunge lasifu mradi vijana kukabili VVU

**Na Mwandishi Wetu,** KILOMBERO

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI imeipongeza serikali kwa ubunifu wa miradi inayosadia vijana kuwajengea uwezo wa kujiamini na kuimarisha uchumi wao ili kujikimu kimaisha wakiwa salama dhidi ya maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dk. Alice Kaijage, alisema juzi kuwa hatua ya serikali kuanzisha miradi hii ukiwamo Mradi wa Timiza Malengo wenye lengo la kuwasaidia wasichana rika balehe na wanawake vijana wenye umri wa miaka 10 hadi 24 na waliopo nje ya shule kuwezeshwa kijamii na kiuchumi ili kujikimu kimaisha, ni muhimu katika kukabiliana na VVU na UKIMWI.

"Kila mmoja anatambua kuwapo maambukizi ya VVU lakini hatua hii inayochuliwa na serikali kupitia Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) ya kukinga vijana wa taifa hili ni jambo la kupongezwa sana.

"Sisi kama wabunge, wito wetu ni kuendelea kuishauri serikali kuongeza bajeti ili vijana wengi wa nchi hii waweze kunufaika," alisema.

Dk. Kaijage aliongeza kuwa matokeo ya Mradi wa Timiza Malengo yanaonekana kwa macho kwa kuwa vijana walionufaika kupitia mradi huo, wanaendelea kukua kupitia mtaji mdogo wanaopatiwa.

Baadhi ya vijana waliotembelewa na kamati hiyo ambao tayari wanaendesha miradi, wameweza kuwahamasisha vijana wenzao na kujiunga katika vikundi kwa lengo la kujipatia mikopo ya serikali ili kuendelea kujikwamua kiuchumi.

Pia walieleza jinsi wanavyofaidika na mradi katika kujikomboa kiuchumi. Vijana hao hupatiwa Sh. 250,000 za Kitanzania ambazo zimewasaidia kuanzisha miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufugaji, kilimo, biashara, kulea na kusomesha watoto wao bila kuwa tegemezi, pia wameunda vikundi vya wasichana wenzao ambavyo vinaweza kuwapa sifa za kupata mkopo wa halmashauri.

Mkuu wa Wilaya ya Kilomberao, Hanji Godigodi, alisema mradi huuo una manufaa makubwa katika Mkoa wa Morogoro kutokana na mafanikio yanayoendelea kuonekana kwa vijana wote waliopo kwenye mradi.

"Mradi huu umesaidia sana vijana lakini naomba kupitia mradi huu, kununuliwe runinga na kuandaliwa CD ambazo zina mafunzo ambayo wanafunzi wakiandaliwa utaratibu wa kuangalia runinga hizo kwa utaratibu wa shule husika na kupatiwa mitihani inayoendana na mada husika, itawasidia kuwajengea ufahamu zaidi na kufuatilia namna sahihi ya kujikinga na maambukizi ya VVU pamoja na magonjwa mengine yatokanayo na ngono," alishauri.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu, Kaspar Mmuya, aliwashukuru wakazi wa Ifakara ambao wameupokea mradi huo na kutekeleza kwa vitendo malengo yake ambayo ni kupambana na vikwazo vinavyowakumba wananchi za hali duni ya kimaisha.

Kaspar alisema mwaka huu serikali imeanzisha mpango rasmi wa kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya VVU kwa wanafunzi wote walio katika shule za serikali na binafsi, katika halmashauri 18 nchini kwa kuwa watoto walio katika rika balehe ndiyo walio katika mazingira hatarishi ya kupata maambukizi ya VVU.

Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko, alifafanua kuwa wakati wanaanzisha mradi huo wa Timiza Malengo, kiwango cha maambukizi mapya ya VVU kilikuwa kikionyesha asilimia 40 ya maambukizi mapya yalikuwa yanatoka kwa vijana walio katika umri wa miaka 15 hadi 24 na kundi hilo la vijana asilimia 80 ni wa kike ambao ni wasichana balehe na wanawake vijana.

Mradi wa Timiza Malengo unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya serikali, AMFREF na TAYOA ukiratibiwa na TACAIDS kwa ufadhili wa Mfuko wa Dunia wa Kupambana na VVU na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria.

# PM ataka waliowakopa wakulima wakamatwe

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa ameagiza wanunuzi wote ambao wamechukua tumbaku kwa wakulima na hawajawalipa fedha zao, wachukuliwe hatua za kisheria ikiwemo kufikishwa mahakamani.

Majaliwa alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na viongozi wa vyama vikuu vya ushirika, AMCOS na wakulima wa tumbaku kutoka wilaya za Urambo na Kaliua, mkoani Tabora.

"Tumbaku katika mkoa wa Tabora ni uchumi, hivyo viongozi kuanzia ngazi ya wizara, mkoa, wilaya, kata na hata vijiji simamieni ushirika kwenye maeneo yenu, ushirika ni uchumi. Sote tuwajibike kwa pamoja, tuhakikishe ushirika unapata mafanikio," alisema.

Waziri Mkuu alisema serikali haitasita kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote atakayebainika kuhujumu ushirika nchini kwa sababu imedhamiria kuuboresha.

Aliwaagiza viongozi wa vyama vikuu vya ushirika waende kwa wakulima na kushirikiana nao kutatua matatizo yao.

"Kutaneni na viongozi wa mkoa na wilaya na muwaeleze changamoto zenu, viongozi wa Serikali nanyi wapokeeni na muwasikilize," alisema.

Pia aliwataka viongozi wa serikali kuanzia ngazi ya kijiji wasimamie mwenendo wa ushirika katika maeneo yao na wahakikishe kwamba hakuna migogoro, wizi wala dhuluma kwa wakulima.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amedhamiria kuendelea kusimamia ushirika wa mazao mbalimbali likiwamo la tumbaku, hivyo aliwasisitiza viongozi hao waongeze usimamizi ili kuimarisha maisha ya wakulima wa zao hilo.

Majaliwa alisema kitendo cha viongozi wa AMCOS kwenda kwa Waziri Mkuu na kuwasilisha kero zao wakati katika maeneo yao kuna viongozi, kinaonyesha kwamba kuna shida, hivyo kuwataka viongozi wa halmashauri watekeleze majukumu yao ipasavyo.

**"Kutaneni na viongozi wa mkoa na wilaya na muwaeleze changamoto zenu, viongozi wa Serikali nanyi wapokeeni na muwasikilize," alisema.**

# Watoto mitaani wamsimulia waziri magumu wanayopitia

**Na Mwandishi Wetu**

BAADHI ya watoto wa mitaani wameeleza masahibu wanayopitia katika maisha yao ya kila siku yakiwamo kutumikishwa kwa ujira mdogo, kufanyiwa vitendo vya ubakaji na ulawiti, na kujihusisha na matumizi ya dawa za kulevya na uvutaji bangi.

Mambo mengine wanayopitia ni kujiunga na vijana kufanya vitendo viovu ikiwamo wizi na kupata magonjwa mbalimbali ambayo yanahatarisha afya na kupoteza ndoto za maisha yao ya baadaye

Watoto hao waliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya kushtukiza aliyoifanya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, maeneo ya Ubungo, Dar es Salaam.

Ziara hiyo ya Dk. Gwajima ni sehemu ya mpango wa serikali wa kuwarejesha watoto wa mitaani kuungana na familia zao ili kupunguza wimbi la ongezeko la watoto hao kwenye maeneo ya mijini.

Mpango huo wa serikali una lengo la kuhakikisha watoto hao wanapata malezi stahiki katika familia zao pamoja na haki zao za msingi kama vile elimu.

Katika ziara hiyo, Waziri Gwajima alikutana na kikundi cha watoto wa mitaani wanaoishi na kuombaomba maeneo ya barabara na kulazimika kulala pembezoni mwa barabara ikiwamo juu ya miti kwa kufunga viota na kulala mithili ya ndege.

Akizungumza na watoto hao wenye umri kati ya miaka 12 na 17, Waziri Dk. Gwajima alibaini kuwa watoto hao wamechoka kuishi maisha ya kuombaomba na wako tayari kurejea mikoa waliyotoka ili kuungana na familia zao.

Waziri aliwataka watoto wote wa mitaani walioko maeneo mbalimbali nchi nzima kutoa ushirikiano kwa maofisa maendeleo ya jamii ili serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wakiwamo wamiliki wa vyombo vya usafiri na Jeshi la Polisi kuwasafirisha ili waungane na familia nyumbani wanakotoka.

Dk. Gwajima aliwataka wazazi kusikiliza ndoto za watoto wao na kubaini wanachohitaji ili wasome na kufikia malengo yao badala ya kuwapotezea malengo waliyo nayo.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula aliwachukua watoto hao zaidi ya 20 na kuwapeleka nyumba ya makao maalum ili kupatiwa ushauri nasaha, kuwaandaa kisaikolojia, kupatiwa huduma za afya na kuandaliwa kwa ajili ya kusafirishwa kurejea kwa wazazi ili kuungana na familia

Watoto hao walisema kuwa baadhi ya watoto wanakimbia familia zao na kujiunga na maisha ya kuwa na watoto wa mitaani si kwa sababu wazazi hawana uwezo au wamefariki dunia.

Walibainisha kuwa migogoro iliyoko kwenye familia, mfano wazazi kutengana, migogoro ya urithi ambayo inasababisha watoto wakimbilie mitaani ili kuepuka kuishi na mzazi wa kambo au kwa ndugu badala ya kuishi na wazazi wao.



WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, akizungumza juzi na mmoja wa watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani, Dar es Salaam, alipofanya ziara ya kushtukiza ikiwa ni sehemu ya kufanya utaratibu wa kuwanusuru kwa kuwarudisha kwenye familia zao. **PICHA: WMJJWM.**

# Waziri: Mabadiliko ya mitaala kuboreha elimu

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

SERIKALI imesema inaendelea kufanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na mabadiliko ya mitaala ili kuongeza ubora wa elimu na mafunzo.

Mapitio hayo ya mitaala na sera, yanaangazia kwa karibu Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ili wakati utatuzi wa changamoto ukiendelea, serikali iangalie nini kifanyike ili kuboresha elimu ujuzi kwa wanafunzi wakiwamo watu wazima.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, aliyasema hayo jana wakati wa hafla fupi ya ufungaji wa mafunzo ya Baraza la Usimamizi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) Kampasi ya Morogoro.

Prof. Mkenda alisema taasisi hiyo inapaswa kushiriki kikamilifu katika utoaji wa maoni ikiwa ni pamoja na kushirikisha kwa karibu wadau wengine kutoa maoni namna ya kuboresha taasisi hiyo hususani katika maeneo ya ujuzi.

Pia alisema Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatekeleza maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa kuhusu kuhakikisha Watanzania waliokosa fursa ya kusoma kutokana na matatizo mbalimbali wanaendelea na masomo.

"Serikali itaendelea kuisaidia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ili kuratibu na kusimamia vyema urahisi wa wananchi kupata fursa ya elimu, hivyo ili kukamilisha jambo hilo itaendelea kuimarisha miundombinu ikiwemo ukarabati na ujenzi wa majengo ya taasisi.

"Majengo ni muhimu lakini elimu si majengo pekee. Tunaweza kutumia muda mrefu kwenye majengo, serikali italeta hela kwa ajili ya majengo lakini kama hatukuweka weledi kwa watu hatuwezi kufika," alisema.

Waziri Mkenda alimtaka Mwenyekiti wa Baraza la TEWW, Dk. Naomi Katunzi, pamoja na wataalamu kufanya ziara Ujerumani ili kujionea taasisi ya elimu ya watu wazima nchini humo inavyofanya kazi ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji.

Naye Dk. Katunzi alimpongeza Prof. Mkenda kwa usimamizi madhubuti wa baraza hilo pamoja na mabadiliko makubwa ya utendaji yanayofanyika katika wizara.

Alisema mafunzo hayo yanayotolewa chini ya Chuo cha Uongozi pamoja Ofisi ya Msajili wa Hazina yamejikita katika kuwaongezea ufanisi wa kiutendaji na uwajibikaji serikalini ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanaacha alama na kielelezo bora katika uwajibikaji.

Mwenyekiti huyo alizitaja changamoto zinazoikabili taasisi hiyo kuwa ni pamoja na ukarabati wa majengo chakavu ikiwa ni sambamba na ujenzi wa majengo mapya kwa ajili ya ofisi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga, Azam kila la kheri mashindano CAF

**MSIMU** mpya wa mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho katika hatua ya awali yanatarajiwa kufanyika kuanzia leo katika viwanja mbalimbali hapa barani Afrika.

Tanzania katika mashindano hayo yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), inawakilishwa na jumla ya timu sita, nne kutoka Bara na klabu nyingine mbili kutoka Zanzibar.

Kwa upande wa Tanzania Bara, Simba na Yanga zote za Dar es Salaam zinatarajiwa kuanza kupeperusha bendera zake leo katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Azam FC ya jijini pia na Geita Gold FC ya mkoani Geita zenyewe zitachuana kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Zanzibar katika michuano hiyo ya kimataifa itawakilishwa na KMKM inayoshiriki Ligi ya Mabingwa Afrika na Kipanga FC wao watapambana kuwania ubingwa wa mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Katika kuhakikisha zinakwenda kushindana na si kusindikiza wengine, timu zote hizo zimefanya usajili mzuri kwa kuzingatia mapungufu waliyoyaona katika msimu uliopita, maana yake wameimarisha vikosi vyao kabla ya kuanza kwa msimu mpya.

Wawakilishi hawa wamefanya pia maandalizi yanayostahili katika kipindi cha Pre Season, lakini pia walicheza michezo mbalimbali ya kirafiki dhidi ya timu za ndani na nje ya nchi ili kujiweka imara na tayari kwa mapambano hayo.

Mbali na mechi hizo za kirafiki, kwa upande wa Simba, Yanga, Azam na Geita Gold zimepata nafasi ya kucheza mechi tatu za Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo zitakuwa ni sehemu ya maandalizi kuelekea michuano hiyo ya CAF, ambapo makocha wanaweza kutumia michezo hiyo kuimarisha wachezaji pale walipobaini kuna matatizo.

Timu zote nne zimepata mechi ngumu kwa sababu kila timu walizokutana nazo zilikuwa zinahitaji kuvuna pointi, hivyo kwa maana nyingine zimewapa maandalizi mazuri wawakilishi hao wa nchi katika mashindano ya kimataifa.

Pia kwa upande wa Zanzibar, KMKM na Kipanga zimepata nafasi ya kushiriki michuano maalumu ya Pre Season na vile vile zimecheza mechi moja za ligi, na kwa umuhimu wake, ilitumia nyota wake wote muhimu kuwaweka tayari kwa sababu zilifahamu majukumu ya kimataifa yaliyokuwa mbele yao.

Tunawakumbusha wachezaji wa timu zote sita kucheza kwa bidii, kujituma wakati wote na kufahamu wanatakiwa kutumia michuano hiyo kutimiza ndoto zao za kupata klabu za nje na hatimaye kuongeza idadi ya nyota wa Tanzania wanaocheza soka la kulipwa.

Wachezaji wafahamu wanatakiwa kupambana kusaka matokeo chanya katika mechi hizi za kwanza na kujiweka kwenye nafasi nzuri kuelekea michezo ya marudiano, haijalishi timu inaanzia nyumbani au ugenini.

Lakini kama ambavyo tumeshuhudia klabu za Tanzania zikisajili wachezaji waliofanya vizuri na wapinzani waliocheza nao, huu ni wakati mwingine sahihi wa nyota wa Kitanzania kujiweka sokoni na hatimaye kuwavutia makocha wa timu za nje. Tunaamini kama Simba, Yanga na Azam zinasajili kutoka kutoka Uganda, Rwanda, Kenya, Zambia, Malawi au Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), tunataka kuona timu za nje nazo kupitia michuano ya msimu huu zinavutiwa na wachezaji Watanzania kama vile walivyosajiliwa kina Mbwana Samatta, Simon Msuva, Thomas Ulimwengu, Kelvin John, Abdi Banda na wengineo. Timu inapopata ushindi katika mechi yake ya kwanza hupunguza presha kwa wachezaji, benchi la ufundi na mashabiki wake kuelekea mchezo wa marudiano ambao tayari kila mmoja anakuwa ameshamfahamu vyema mpinzani wake.

Tunafahamu kila hatua huwa na dakika 180, lakini ni vyema kila klabu ikajidhatiti kuhakikisha inamaliza kazi ndani ya dakika 90 za kwanza na kuacha muda uliobakia kuwa mwepesi na si wenye mawazo.

Tunawakumbusha hivi kwa sababu tunahitaji kuona timu za hapa nchini zinafika mbali katika mashindano hayo na kufuta usemi uliozoeleka wa 'Kichwa cha Mwendawazimu' na kuonekana klabu za Tanzania ni tishio.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Kweli Mchengerwa, Taifa Stars inahitaji mabadiliko

Na Adam Fungamwango

**N**I juzi tu hapa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, alitaja baadhi tu ya mabadiliko yanayopaswa kwa ajili ya kuijenga upya Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), baada ya kufanya vibaya katika mechi za kusaka tiketi ya kucheza fainali za wachezaji wanaocheza Ligi za Ndani Afrika (CHAN).

Stars ilishindwa kufuzu CHAN baada ya kuchapwa jumla ya mabao 4-0, ikikubali bao 1-0 nyumbani na kufungwa mabao 3-0 ugenini nchini Uganda, dhidi ya wenyeji, The Cranes. Si tu Taifa Stars ilifungwa, lakini pia kwenye mechi zote mbili haikucheza vizuri kitu ambacho kiliwafanya mashabiki wengi wa soka nchini kupaza sauti wakitaka kitu kifanyike kwa ajili ya kuisuka upya.

Moja kati ya vitu alivyovitaja vitafanyika ni serikali kuchukua jukumu la kumlipa kocha ili kupatikana kwa mwalimu mwenye uwezo mkubwa kama ilivyokuwa zamani.

"Jambo la kwanza ni makocha, lazima tuwe na makocha wazuri, tunataka makocha wenye ujuzi mkubwa na si wa kawaida. Zamani kulikuwa na makocha walikuwa wakifanya vizuri sana kwa sababu serikali ilikuwa inawagharamia, alisema waziri huyo.

Lingine alisema ametoa siku 14 kwa baadhi ya watu waliowapa kazi wamletee taarifa ili kujua wachezaji wazuri walipo na hakuna tena sababu ya kuwa na mchezaji kuwamo kwenye kikosi cha timu ya taifa ambaye hajitumi hata kama ana jina kubwa kiasi gani.

"Katika mambo tuliyoyagundua watu wetu ni wavivu, lakini pia watu wetu hawajitumi, kwa sababu katika michezo hii miwili iliyochezwa, utagundua tu watu wetu hawajitumi na sisi kama wizara tunaangalia ni hatua gani ambazo tunaweza kuchukua. Nimeagiza siku 14 wanileteе taarifa ili tujue mchezaji gani yupo wapi, wale ambao tunaona hawafanyi vizuri, hakuna tena sababu ya kuwa na mchezaji hata kama ana jina kubwa kuwamo kwenye kikosi cha timu ya taifa."

Ukiangalia anayosema Mchengerwa, ni wazi kabisa kuna baadhi ya wachezaji walionyesha wanacheza mpira wa kawaida sana kwenye zile mechi mbili japo majina yao ni makubwa katika medani ya soka.

Utashangaa kuona mchezaji anayecheza vile kwenye kikosi cha timu ya taifa, ndiyo yule ambaye anajituma na kupambana akiwa katika klabu yake.

Kwa wachezaji wa wenzetu nje ya nchi, mchezaji kucheza kwenye timu ya taifa ni fahari, yupo tayari kuandika barua ya kuhama kama hapati namba kwenye timu kubwa, aende kucheza timu ndogo itakayompa nafasi ya kucheza kwa sababu tu ili achaguliwe kucheza katika kikosi cha taifa lake.

Huu unaitwa ni ukosefu wa uzalendo. Haiwezekani mchezaji anacheza hadi tone la mwisho la damu yake, lakini akiwa kwenye kikosi cha Stars anacheza kawaida sana ili tu kutimiza wajibu ili dakika 90 zimalizike.

Pamoja na kwamba udhaifu wa Stars ni matatizo mtambuka, lakini inashangaza kuona hata kuteua kikosi bado ni tatizo.

Mara nyingi kikosi huteuliwa kutokana na wachezaji waliofanya vyema kwa kipindi hicho. Lakini Stars inaweza kuchagua wachezaji ambao wapo siku zote hata kama kwenye klabu zao hawachezi, au viwango vyao vimepungua na wakiwa kwenye timu ya taifa hawajitumi. Na kuna wachezaji ambao wanakuwa wamefanya vyema kwenye kipindi hicho, lakini hawachaguliwi. Hili linaifanya timu kudumaa kuwa na wachezaji ambao hawapambanii namba kwani wanajua wataitwa tu kutokana na ustaa wao na hata wakifika huko wanacheza pia kistaa.

Wakati mwingine mpaka mashabiki wapige kelele mchezaji fulani hajachaguliwa, ndipo achaguliwe.

Wachezaji wa Kitanzania nao wana tatizo la kutokuwa na mwendelezo. Leo atacheza hivi kesho vile. Hii nayo inawapa tabu sana makocha wa timu ya taifa kuchagua.

Bado kama nchi hatuna wachezaji angalau sita au saba hivi wa viwango vya juu wanaocheza nje ya nchi.

Wachezaji wetu wamebweteka nchini hadi wapo baadhi ya watu wanapigania kutengenezea kanuni ya kuwalinda kwa kupunguza wachezaji wa kigeni, wakati nao hawajafungiwa milango wanatakiwa watoke waende nje ya nchi kwa maslahi yao na timu ya taifa.

Pia namwomba waziri aangalie sasa uwezekano kuna kwenda bungeni kupigania itungwe sheria ya uraia pacha angalau kwa wanamichezo tu, ili tupate Watanzania waliozaliwa nje au wenye uraia wa nchi mbili waitumikie Stars. Kama nilivyosema matatizo ya Stars ni machache sana na ni mtambuka, kwa leo ni haya niliyoyabainisha na wanamichezo sasa tumuunge mkono Mchengerwa ili atekeleze majukumu yake vyema, husuan la kuifanyia mabadiliko timu ya taifa akishirikiana na Shirikisho la Soka Nchini (TFF).

# Rais China, Mwenyekiti AU watumiana pongezi miaka 20 ya Umoja wa Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa China, Xi Jinping na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika (AU), Macky Sall, jana walibadilishana salamu za pongezi kwa kuadhimisha miaka 20 tangu kuanzishwa kwa umoja huo na uhusiano wa kidiplomasia kati yake na nchi hiyo.

Katika salamu hizo, alizokaririwa na Shirika la Habari la China (Xinhua) Rais Xi alisema katika miaka 20 iliyopita, AU imeziongoza nchi za Afrika katika kupiga hatua kutafuta nguvu kupitia umoja, maendeleo, uhuishaji na utangamano. Pia alisema AU, imezisaidia nchi hizo kuonyesha nguvu za Afrika katika kupambana na janga la UVIKO-19, kuunga mkono ushirikiano wa pande nyingi kulinda maslahi ya pamoja ya nchi zinazoendelea.

Alibainisha kuwa China na Afrika siku zote zimekuwa marafiki wazuri, washirika na ndugu wazuri wanaoshirikiana kwa pamoja na kwmaba uhusiano kati ya China na AU umekuwa mtihani wa mabadiliko katika nyanja za kimataifa na ushirikiano kati ya nchi hizo mbili umepanuka kwa kina na mapana na kuwa kiongozi muhimu jukumu la kuendeleza urafiki wa jadi kati ya China na Afrika na kuimarisha mshikamano na ushirikiano katika enzi mpya. Xi, alisema anatilia maanani maendeleo ya uhusiano kati ya China na AU, yuko tayari kufanya kazi na Rais Sall, na wakuu wengine wa nchi wanachama wa AU ili kuanza mwanzo mpya wa miaka 20 ya uhusiano wa kidiplomasia kati ya China na AU kuendeleza moyo wa ushirikiano wa kirafiki kati ya China na Afrika.

Alisema, masuala mengine ya ushirikiano ni kutekeleza kikamilifu matokeo ya Mkutano wa Nane wa Mawaziri wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC), kuunga mkono kithabiti masuala yanayohusu maslahi yao ya msingi na mambo yanayohusu mambo makuu kuongeza uwakilishi na sauti ya nchi zinazoendelea katika masuala ya kimataifa na kutoa mchango mpya katika ujenzi wa jumuiya ya China na Afrika yenye mustakabali wa pamoja katika enzi mpya.

Naye Sall, ambaye ni Rais wa Senegal, alisema Rais Xi ametuma salamu za pongezi kwa kuadhimisha miaka 20 tangu kuanzishwa kwa AU, ambayo imedhihirisha kikamilifu urafiki wa karibu kati ya watu wa Afrika na China na kutoa shukrani zake za dhati kwa Xi.

Rais Sall, alisema anatamamani sana urafiki wa jadi, mshikamano na ushirikiano kati ya Afrika na China, pamoja na ushirikiano wenye nguvu chini ya mfumo wa FOCAC.

Sall, alikaririwa alisema Afrika inaunga mkono kithabiti kanuni ya kuwa na China moja na pia, anaunga mkono bara la Afrika kufanya kazi na China rafiki ili kujenga jumuiya ya China na Afrika yenye mustakabali wa pamoja katika enzi mpya.



Wafanyabiashara waliokuwa wakifanya shughuli zao kwenye eneo la mwekezaji, Temeke Vetenari, mkoani Dar es Salaam, wakihamisha bidhaa zao jana, kupisha kuvunjwa kwa vibanda vyao ili kupisha ujenzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Polisi washtuka mauaji wapenzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUTOKANA na kukithiri kwa matukio ya mauaji ya wapenzi, Jeshi la Polisi mkoani Dodoma limeanza kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya uhusiano, kundi la vijana likipewa kipaumbele,

Hatua hiyo imechukuliwa kutokana na kushamiri kwa matukio hayo, ndani ya juma hili pekee kukiwa na matukio mengi ya mauaji ya wapenzi, likiwamo la juzi mwanafunzi wa Chuo cha St. John, Winifrida Michael (24), aliyeuawa kwa kuchomwa kisu na na mwanafunzi na mpenzi wake (26).

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Martin Otieno, akizungumza jijini hapa jana, alisema jeshi hilo litashirikiana na wakazi wa mkoa huo kuelimisha vijana kuhusu masuala ya uhusiano ili wawe na tahadhari kabla ya kuingia kwenye uhusiano wa aina hiyo.

"Pale unapokuwa tayari unaona kwamba ni mtu ambaye unaweza kuwa na uhusiano, basi tujitahidi zinapotokea tofauti za hapa na pale, ni vizuri kutafuta mwafaka ili maisha mengine yaendelee.

"Kama mnashindwana kabisa, ni bora mkaachana kila mtu akaendelea na biashara zake kuliko kuchukua uamuzi wa kuuana na kujeruhiana," alishauri. Akizungumzia mauaji ya mwanafunzi huyo, Kamanda Otieno alisema tukio hilo liliripotiwa Septemba 7, mwaka huu majira ya saa nne usiku katika Mtaa wa Kikuyu Mission ambapo Winifrida alikuwa anasomea stashahada ya maabara kwenye chuo hiko.

"Winifrida aliuawa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali tumboni na mtuhumiwa Julius Gervas (26), kiini cha tukio kinasadikiwa kuwa wivu wa kimapenzi, hivyo mtuhumiwa amekamatwa ila kwa sasa yupo katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma akiendelea kupatiwa matibabu.

"Baada ya kufanya tukio la mauaji, alijifungia kwenye chumba cha Winifrida na kujijeruhi kwa kutumia kitu chenye ncha kali maeneo ya tumboni lakini tuliwahi. Kwa hiyo, mpaka sasa anaendelea kupatiwa matibabu na tunaendelea na uchunguzi ili akipata nafuu, hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake kwa kufikishwa mahakamani," alisema.

Muuguzi Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Stanley Mahundo, alithibitisha mtuhumiwa huyo anapatiwa matibabu hospitalini huko huku akitoa wito kwa jamii kuhakikisha haitumii silaha zenye ncha kali wanapokuwa na mikwaruzano.

## Tatizo mbegu sasa lawekewa mkakati

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imeweka mikakati ya kumaliza uhaba wa mbegu kwa wakulima nchini baada ya kutenga Sh. bilioni 40 kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu bora za kisasa.

Hatua hiyo itachochea ukuaji wa sekta ya kilimo kutoka asilimia 4.5 ya sasa hadi asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

Waziri wa Kilimo, Husein Bashe, alisema hayo juzi wakati akizungumza katika siku ya Maonesho ya Wakulima katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzani (TARI) Kituo cha Ilonga, Kilosa mkoani hapa.

Alisema, kupitia mpango huo, serikali imeshaziagiza taasisi zake, ikiwamo TARI Ilonga kutatua tatizo hilo.

TARI Ilonga, ilifanya maonesho ya wakulima kupitia mradi wa uendeshaji na upatikanaji wa mbegu za mazao ya jamii ya mikunde na nafaka Afrika (AVISA) yaliyowakutanisha maafisa kilimo kutoka katika kata zote za wilaya ya Kilosa.

Katika hotuba yake iliyosomwa na Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Richard Semango, Bashe alisema, lengo la kuongeza uzalishaji wa mbegu ni kuwawezesha wakulima kutumia mbegu na teknolojia za kisasa kuongeza tija katika mazao ili kukuza uchumi kupitia kilimo.

Alisema, uzalishaji huo mbegu za teknolojia za kisasa utafanywa na watafiti kutoka TARI kupitia vituo vyake vyote nchini na mbegu hizo zitasaidia kuhimili changamoto mbalimbali ikiwamo mabadiliko ya tabianchi.

Kaimu Mkurugenzi TARI Ilonga, Emmanuel Chilagane, alisema lengo la maonyesho hayo ni kuhamasisha wakulima kuanza kutumia mbegu bora zilizofanyiwa utafiti wa kitalaamu ili kuongeza tija katika mazao jamii ya mikunde na kuongeza mnyororo wa thamani katika soko la kitaifa na kimataifa.

Alisema TARI Ilonga, imekuwa ikivumbua teknolojia za mazao mbalimbali kwa kuzalisha mbegu za awali na kuzipeleka kwa kampuni mbalimbali za kuzalisha mbegu ili zizalishe kwa wingi na kuleta tija kwa wakulima.

Naye Meneja Uhaulishaji Teknolojia Biashara na Uhusiano kutoka TARI, Makao Makuu, Magreth Mchomvu, alisema msisitizo mkubwa wa serikali kwa wakulima ni matumizi ya mbegu bora zilizofanyiwa utafiti ili kuongeza uzalishaji.

Mratibu wa Mradi wa Kitaifa wa Mradi wa AVISA, Emmanuel Mwenda, alisema mradi huo unatekelezwa katika nchini saba na hapa nchini katika vituo vinane vya TARI katika mazao yakiwamo ya maharage, mtama, kunde, mbaazi na dengu.

Mtafiti Mwandamizi wa Mazao ya mikunde wa TARI Ilonga, Meshack Makenge, alisema kwa sasa mazao ya mikunde yameshapata soko la uhakika lakini changamoto ni uzalishaji mdogo.

# Wanafunzi 24,000 hawana madawati

**Na Said Hamdani,** LINDI

ZAIDI ya wanafunzi 24,260 kati ya 265,488 wanaosoma shule mbalimbali za msingi na sekondari mkoani Lindi, wanalazimika kuketi sakafuni wakati wa masomo kutokana na upungufu wa madawati unaozikabili shule zao.

Mshauri wa Elimu mkoani humo, Vicent Kayombo, alibainisha hayo juzi wakati wa kikao kazi cha elimu kilichojumuisha wadau wa elimu, wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, maofisa elimu kata na wakuu wa shule mjini Lindi.

Akiwasilisha taarifa yake, Kayombo alisema tatizo la wanafunzi kuketi sakafuni wakati wa masomo yao, wamelikuta katika shule mbalimbali za msingi na sekondari walipokuwa kwenye ziara za kufanya ukaguzi kuangalia kazi za ufundishaji zinazofanywa na walimu na vikwazo vilivyopo.

Alisema katika ukaguzi huo, wamebaini shida zingine zikiwamo baadhi ya maofisa elimu kata kutowajibika ipasavyo, akiwamo waliyemkuta akiwa na mfuko wa maboga akitoka shambani muda wa kazi za kiserikali na aliwakimbia baada ya kuwaona.

"Tukiwa njiani kuelekea kwake tukautana naye amebeba mfuko wa maboga alitukimbia kuelekea porini. Huyo ni ofisa elimu kata," alisimulia Kayombo.

Alizitaja baadhi ya shule ambazo wanafunzi wake wanaketi chini na idadi kwenye mabano ni Kivinje, Njia Nne na Somanga wilaya ya Kilwa (wanafunzi 2,944), Namangale, Mbagala na Mmongomongo katika Halmashauri ya Mtama (747).

Zingine ni Kibutuka na Ruza Mlelwa za Halmashauri ya Liwale (336), Stadium na Kiwawa ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi (308) pamoja na Kaloleni na Uhuru za wilayani Nachingwea (294).

Mshauri huyo wa elimu alisema tatizo la upungufu wa madawati, meza na viti lipo kwa kila shule za msingi na sekondari katibu Mkoa wa Lindi.

Katibu Tawala Mkoa wa Lindi, Ngusa Samike, akizungumza katika kikao hicho, alisema hoja zote zilizotajwa, zitaendelea kufanyiwa kazi huku akiwataka wataalamu wa elimu kutimiza wajibu wao.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainabu Telak, aliwataka wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri kutafuta njia za kupunguza tatizo hilo ili wanafunzi wasome katika mazingira rafiki.

# Madiwani wanaume watakiwa kusindikiza wake zao kliniki wakati wote wa ujauzito

**Na Friday Simbaya,** KILOLO

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa, wameshauriwa kuongozana na wake zao kliniki wanapokuwa wajawazito kwa ajili ya kufahamu maendeleo ya mtoto aliyepo tumboni.

Ushauri huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Anna Msolla, wakati wa mkutano wa madiwani wa kawaida alipokuwa anachangia katika kamati ya wilaya ya kudhibiti UKIMWI, ambayo inaongozwa na Hezron Nganyagwa.

Alisema kwa kufanya hivyo, itakuwa mfano kwa wananchi wanaowaongoza katika kata zao kuwa na mwamko wa kuongozana na wake zao kliniki pindi wanapukuwa wajawazito ili kupata ushauri wa kiafya juu ya maendeleo ya mtoto tumboni.

"Ingawa kinababa walio wengi sasa wanajua umuhimu wa kuwasindikiza wazazi wenza (kinamama) kliniki wakati wa ujauzito na hata baada ya kujifungua, bado wako wengi wanadhani kuwa wanatakiwa kwenda huko kwa ajili ya kupima ukimwi tu," alisema.

Msolla alisema, wanaume kwenda kliniki na wake zao watafahamu mambo mengi ambayo pia ni faida kwao na yatasaidia katika makuzi na malezi ya watoto.

"Sote tunawajibika katika makuzi ya mtoto kwa hiyo ni wajibu wa mwenza kumsindikiza mwenzake kwani hilo litaleta ukaribu pia kati ya baba na mtoto aliyeko tumboni," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Msolla, tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa mtoto hushiriki furaha aliyo nayo mama ambapo mama mwenye furaha na mtoto naye anakuwa na furaha angali tumboni.

Wakizungumzia suala la makuzi na malezi, kinababa walio wengi wamedai kukosa nafasi ya kuongozana na wake zao kliniki kutokana na kubanwa na majukumu ya kila siku ya kutafuta riziki.Kwa upande wao baadhi ya wanawake wamesema wanajisikia faraja pale baba anapomsindikiza kliniki.

Wataalamu wa tiba wanasema kwamba, wanaume wengi wametawaliwa na dhana isiyo sahihi kwamba suala la ujauzito ni la mwanamke pekee kwa vile ndiye anayeibeba lakini, wanasema ushiriki wa baba wa muda wote katika afya ya ujauzito ni muhimu na kuna faida kubwa.

Kutokana na kutokujua umuhimu wa ushiriki wao, wanaume wengi wamekuwa na visingizio lukuki ilimradi wasiandamane na wake zao kliniki, lakini wataalamu hao wanasema visingizio vinavyotolewa si vya msingi ukilinganishwa na faida zinazopatikana kwa uwapo wao kwenye huduma za afya tangu mimba inatungwa hadi mtoto kukua.

wamesema kitendo cha mke na mume kuongozana kwenda kliniki ni kizuri, lakini bado jamii hasusani upande wa wanaume hawana uelewa wa jambo hilo, hivyo ameomba serikali na wadau wengine kutoa elimu



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (kulia), akiangalia moja ya vitabu vilivyoingizwa nchini na kampuni ya Big Bad Wolf, katika ufunguzi wa maonyesho na mauzo ya vitabu hivyo, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mwanzilishi wa Big Bad Wolf, Andrew Yap (katikati) na Mwakilishi wa kampuni hiyo nchini, Mohamed Noor. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waziri Nape Nnauye apigia debe vitabu bei chee

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Nape Nnauye, amewataka wamiliki wa shule kuchangamkia fursa ya maonyesho ya vitabu yanayoendelea jijini Dar es Salaam ili kupata vitabu mbalimbali wanavyovihitaji.

Nape, aliyasema hayo jana kwenye ukumbi wa Diamond Jubele, jijini Dar es Salaam, wakati wa ufunguzi wa maonyesho na mauzo ya zaidi ya vitabu 500,000 vilivyoingizwa nchini na kampuni ya Big Bad Wolf.

Alisema kampuni hiyo imeleta vitabu vya kila aina, hivyo Watanzania hususan wamiliki wa shule za msingi na sekondari, wanapaswa kuichangamkia fursa hiyo kupata mahitaji yao ya vitabu.

"Mimi mwenyewe nimevutiwa sana na maonyesho haya na nitawaleta watoto wangu waje kuangalia vitabu wanavyovipenda. Wana vitabu vingi sana ambavyo ukienda kwenye maduka mengine bei yao ni mara tatu ya wanayouzia hapa," alisema Nape.

Alipongeza kampuni hiyo kwa uamuzi wa kuja na vitabu hivyo Tanzania kwa kuwa vitasaidia kuongeza ufahamu na ujuzi kwa watanzania wengi ikiwemo kuongeza chachu ya utamaduni wa kusoma.

Waziri Nape, alisema kuna Watanzania wengi wanaoagiza vitabu kutoka nje ya nchi, hivyo ujio wa vitabu hivyo ni fursa kwao kuzungumza na kampuni hiyo namna wanavyoweza kushirikiana katika biashara hiyo. "Mimi ni mbunge nafahamu ilivyo shida kupata vitabu vya kutosheleza shule zetu. Sasa niwashauri wenye shule kama wameletewa vitabu vyote hivi hapa Tanzania nadhani ni fursa adhimu kwao kuja kuangalia na kuchukua vitakavyowafaa," alisema.

Maonyesho hayo, alisema yatawasaidia Watanzania kujenga utamaduni wa kusoma vitabu kwa kuwa watu watakaofika kwenye maonyesho hayo watapata vitabu wanavyopendelea.

Nape alisema, kampuni hiyo imeahidi kuwa kila mwaka itakuwa inaleta vitabu hivyo na kufanya maonyesho ya aina hiyo ili kuwapa fursa watanzania kupata vitabu wanavyovihitaji kwa gharama nafuu.

Kampuni ya Big Bad Wolf, inayojulikana kwa uuzaji wa vitabu duniani, iliingiza nchini vitabu 500,000 hivi karibuni ikiwa ni mwendelezo wa jitihada za kujenga kizazi kipya cha wasomaji wa vitabu.

Mwanzilishi Mwenza wa vitabu vya Big Bad Wolf, Andrew Yap, ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Big Bad Wolf Sharjah, alisema walifurahishwa na kupendezwa kuleta mauzo ya vitabu nchini Tanzania kwa mara ya kwanza baada ya kuona kuna soko kubwa na wepesi wa kuingia.

"Kwa hakika ni hatua ya kusisimua na muhimu kwetu katika vitabu vya Big Bad Wolf, tuliposafiri kuelekea Afrika, na kuja Tanzania kama kimbilio letu la kwanza. Dhamira yetu kuu siku zote imekuwa kukuza mazoea ya kusoma Kiingereza ulimwenguni kote na kujenga kizazi kipya cha wasomaji kwa kufanya vitabu kuwa bei nafuu na kupatikana kwa kila mtu.

"Pamoja na mada 15,000 zinazopatikana na vitabu 500,000 vipya vya Kiingereza vinavyotolewa, tunataka Watanzania kutoka nyanja mbalimbali wawe vijana au wazee, wagundue furaha ya kusoma na kupata maarifa, bila kujali kiwango cha mapato yao," alisema.

Alisema vitabu vya Big Bad Wolf, vilizinduliwa Kuala Lumpur Malaysia, mwaka wa 2009 na dhamira ya waanzilishi ni kukuza tabia ya kusoma, kuongeza ujuzi wa kusoma Kiingereza ulimwenguni kote.

Alisema, tangu kuanzishwa kwake, uuzaji wa vitabu vya Big Bad Wolf umebadilisha maisha ya watu wengi kwenye nchi za Kambodia, HongKong, Indonesia, Myanmar, Pakistan, Ufilipino, Singapore, Sri Lanka, Korea Kusini, Thailand, Taiwan, Falme za Kiarabu (UAE), pamoja na Malaysia.



# Anatafutwa baada ya kutoweka nyumbani

**Na Magdalena Jackson, SJMC**

MZEE Victory Ladenga (92) Pichani, mwenyeji wa Rombo mkoani Kilimanjaro, anatafutwa baada ya kutoweka nyumbani kwa mtoto wake, Venance, eneo la Kikuyu Magengeni jijini Dodoma.

Akizungumza na Nipashe jana, mkwe wa mzee huyo, Frank Kiza, alisema amepotea ikiwa ni siku moja baada ya kuwasili Septemba 5, mwaka huu, akitokea Rombo.

Kiza alisema baada ya kutoweka mzee huyo, walifanya jitihada za kumtafuta sehemu mbalimbali zikiwamo hospitalini, misikitini, kanisani na vituo vya polisi bila mafanikio.

Alisema baada ya juhudi zote hizo kugonga mwamba, walitoa taarifa kituo cha polisi na kuandikiwa namba DOM/RB/11810/2022.

"Naomba mtu yeyote anayefahamu taarifa zake atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu au kwa kupiga simu 0713 570 189 (Frank) au 0763 756 491 (Venance)," alisema



# Wafurahia ujenzi wa soko la machinga

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAJASIRIAMALI mkoani Dodoma wameipongeza serikali kwa kujenga soko la wazi la machinga litakalosaidia kuondoa adha ya mvua na jua waliyokuwa wakiipata kwa muda mrefu.

Katibu wa Wajasiriamali wa Mkoa wa Dodoma, Christopher Dioniz, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mradi huo uliogharimu Sh. bilioni 9.53. Pamoja na pongezi hizo, Dioniz aliomba uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuhakikisha watu watakaopata nafasi katika soko hilo ni wale wanaostahili na si vinginevyo.

"Mradi huu ni mkubwa sana ambao serikali imewekeza fedha zake. Tunaomba uogozi wa jiji kuhakikisha hakuna upendeleo kwenye kutoa nafasi. Wanaopata nafasi wawe machinga kweli na usifanyike udanganyifu wowote," alisema Dioniz.

Aidha, aliwataka wamachinga kuunga mkono juhudi za serikali kwa kufanya biashara katika eneo hilo na kulipa kodi ili kusadia kupanua wigo wa ukusanyaji mapato ya jiji.

"Huu ni mradi ambao utakuwa chanzo kipya cha mapato kwani hivi sasa kumekuwapo na taarifa kuwa jiji la Dodoma limeshuka katika ukusanyaji wa mapato kutokana na biashara ya uuzaji wa viwanja kupungua kasi. Kwa hiyo hiki ni chanzo kipya cha mapato ambacho ni cha kudumu," alisema.

Pia, alisema kukamilika kwa mradi huo kutasaidia wamachinga kukopesheka kutokana na kusajili na kutambulika maeneo yao wanayofanyia biasahara.

"Pia soko hili linakwenda kujibu ukakasi uliokuwapo hapo awali kuwa wafanyabiashara wakubwa wanawatumia machinga kukwepa kulipa kodi ya serikali," alisisitiza Dioniz.

Kadhalika, aliitaka serikali kuweka mfumo thabiti ambayo itasadia kudhibiti upotevu wa mapato na uwekezaji uliofanywa kuonekana kuwa hauna tija kwake na kwa machinga.

Mkurugenzi Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni alisema kutokana na kukamilika kwa mradi huo ambao una uwezo wa kuhudumia zaidi ya wafanyabiashara 5,000 ifikapo Septemba 24, mwaka huu, hakuna machinga yeyote ambaye ataendelea kubaki mtaani.

Alisema, kutokana na miundombinu ya kisasa iliyowekwa katika soko hilo kikiwamo kituo cha polisi pamoja na kamera za ulinzi (CCTV), biashara zitakuwa zinafanyika kwa muda wa saa 24.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (wa tatu kulia), akiangalia kifaranga cha bata mzinga alipotembelea banda la wajasiriamali la wafugaji wa kuku wa kikundi cha Kilasara Mama's, katika kilele cha wiki ya elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo, jijini Dodoma jana. Kulia kwake ni Diwani wa Kata ya Viwandani, Jafari Mwanyemba. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waliokatisha masomo warejea shuleni

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, amesema zaidi ya wanafunzi 50 wa shule za msingi na sekondari waliokuwa wamekatisha masomo kwa sababu mbalimbali, wamerudi shuleni kuendelea na masomo.

Aidha, amesema jitihada kubwa zinaendelea kufanyika kati ya serikali na wadau wa elimu ili kuwarejesha wengine kuendelea na masomo yao. Shekimweri, alieleza hayo jana alipokuwa akizungumza na wananchi kwenye maadhimisho ya Kilele cha Juma la Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo, yaliyofanyika jijini hapa.

Alisema wilaya hiyo imefanikiwa kuwapata watoto hao waliokatisha masomo yao, lakini bado juhudi zaidi zinaendelea kuwatafuta wengine ambao wamekatisha masomo ili waendelee na elimu.

"Wako watoto wengi walioshindwa kuendelea na masomo kwa sababu mbalimbali. Wengine walibakwa, wengine uchumi na wengine ni changamoto ya ujana balehe na wengine kubebeshwa mimba," alisema.

"Kwa maana hiyo niwatake watendaji wa idara ya elimu kwa kushirikiana na wadau wengine kuendelea kutafuta uwezekano wa kuwapata watoto ambao wanahitaji kuendelea na masomo," aliongeza.

Mkuu huyo aliwahimiza wazazi na walezi kuhakikisha wanapeleka watoto wao shuleni kwa wale walioacha kwa kupata ujauzito na watoro ili kuendelea na masomo.

Alisema wako baadhi ya watoto wengi ambao wameshindwa kuendelea na masomo na wengine kukataliwa na mfumo wa kujiunga na elimu ya msingi au sekondari baada kupata ujauzito.

Shekimweri alisema kwa hivi sasa kwa kutumia mfumo wa elimu ya watu wazima wanahaki ya kuendelea na masomo,hivyo wazazi na walezi hakuna sababu ya kutowaendeleza kielimu.

"Ukitaka kuendelea kutawala watu, kuwaone watu na kushindwa kuwapatia huduma muhimu na wasilalamike, wanyime haki ya kupata elimu.

"Lakini kwa kuliona hilo Rais Samia Suluhu Hassan, ametoa maelekezo kuwa watoto wote ambao waliokatisha masomo yao iwe kwa bahati mbaya au kwa changamoto yoyote ya kimaisha kubebeshwa mimba basi wanayo fursa ya kuendelea na masomo sasa," alisema Shekimweri.

Aidha, alisema kitendo cha kuwanyima watoto elimu ni kitendo cha kuwatengenezea umasikini kwani hata maandiko matakatifu yanahimiza kuishika sana elimu.





# Waziri aeleza uhalali wa tume ya pamoja ya fedha Muungano

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk Sada Mkuya Salum, amesema Tume ya Pamoja ya Fedha imeanzishwa kupitia ibara ya 134 ya Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977 na sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha, Sura 140.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi Wingwi Kombo Mwinyi Saleh, aliyetaka kujua lini akaunti ya pamoja itaanzishwa kwa maslahi ya pande zote za Muungano.

Dk. Mkuya, alisema majukumu ya tume yameainishwa katika ibara ya 133 na 134 ya Katiba na kwa mujibu wa sheria ya tume, ni jukumu lake kutoa mapendekezo na ushauri kuhusu uhusiano wa kifedha kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).

Alisema, katika kutekeleza majukumu yake, tume imeandaa na kuwasilisha SMT na SMZ mapendekezo kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano.

Kwa mujibu wa Waziri, kutekelezwa kwa mapendekezo hayo kutawezesha kufunguliwa na kutumika kwa akaunti ya fedha ya pamoja.

Hata hivyo, alisema pande mbili za Muungano zinaendelea na mashauriano na uamuzi utakapofikiwa akaunti hiyo itafunguliwa na kuanza kutumika.

"Kwa kuwa uamuzi bado haujafikiwa na pande mbili za Muungano, utaratibu uliopo ni kwamba mapato ya Muungano yanayokusanywa Zanzibar huwekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya SMZ na kutumika kugharamia uendeshaji wa shughuli za serikali ya Zanzibar," alisema Dk. Mkuya.

Pia, alisema mapato ya Muungano yanayokusanywa Tanzania Bara huwekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya SMT na kutumika kugharamia mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano kwa Tanzania Bara.

Alisema, kila upande wa Muungano umeendelea kunufaika na mapato yanayotokana na misaada na mikopo ya kibajeti kutoka kwa washirika wa maendeleo pamoja na gawio la Benki Kuu ya Tanzania kwa uwiano wa asilimia 4.5 kwa SMZ na asilimia 95.5 kwa SMT.

Waziri huyo alisema SMT imekuwa ikirejesha kwa SMZ mapato ya kodi yatokanayo na kodi ya mshahara (PAYE), inayokusanywa kutoka kwa watumishi wa SMT wanaotekeleza majukumu yao Zanzibar na watumishi wa kampuni na mashirika yaliyosajiliwa Tanzania Bara na kufanya biashara Zanzibar.

"Akaunti ya Fedha ya pamoja itakapofunguliwa na kuanza kutumika, mapato yote ya Muungano yatawekwa katika akaunti hiyo na kutumika kugharamia uendeshaji wa mambo ya Muungano," alisema.

Endapo kutakuwa na bakaa baada ya matumizi kufanyika, alisema bakaa hiyo itagawanywa kwa SMT na SMZ kwa kiasi kitakachoamuliwa na pande mbili za Muungano.



Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Sada Mkuya, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wafanyakazi 243 waajiriwa kwa mkataba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imekiri kuwa katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA), kuna wafanyakazi wa mkataba 243 ambao hawajaajiriwa.

Kwa mujibu wa wizara, watu hao wanafanya kazi katika kada tofauti ndani ya Viwanja vya Abeid Aman Karume, Pemba na Nungwi.

Waziri wa wizara hiyo, Dk. Khalid Salum Muhammed, aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mfenesini, Machano Ahmed Said.

Katika swali hilo, Machano alitaka kujua serikali imechukua hatua gani za kuwaajiri wafanyakazi hao ili kuongeza ufanisi wa kazi katika eneo hilo muhimu.

Waziri Khalid, alisema ZAA imeshaijulisha serikali kupitia wizara yake kuhusu kuwapo wafanyakazi wa mkataba na wizara ilitaka mamlaka hiyo iandae wasilisho ambalo tayari limeshatekelezwa na limeshafika wizarani.

Pia alisema, serikali imechukua hatua ya kuwapanga upya wafanyakazi wake ili kugundua mahitaji halisi ya wafanyakazi kwa taasisi tofauti na kwamba kukamilika kwa kazi hiyo kunaweza kukatoa sura kamili ya mahitaji ya ajira kwa kila taasisi.

" Mheshimiwa Spikia, ni kweli utaratibu wa uchukuaji wa wageni mashuhuri hutumika kwa gari maalum, abiria wa VIP wanaochanganywa na abiria wa kawaida ni kutokana na aina ya tiketi wanayoikata kwa mashirika hayo"alisema.

Aidha, alisema kawaida ya wageni hao mashuhuri hufanya mkataba baina ya Mashirika ya Ndege na abiria wenyewe ili kupata huduma stahiki kulingana na hadhi yao.

Alisema pia, serikali kupitia ZAA imeshafanya mazungumzo na muwekezaji wa kampuni ya DNATA kwa ajili ya kuimarisha.

## Wakunga na wauguzi 100 waajiriwa rasmi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya imesema imeajiri wakunga na wauguzi 100 hatua ambayo itaongeza ufanisi wa kutoa huduma za kinamama na watoto na kupambana na vifo vinavyotokana na uzazi.

Naibu Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidh, alisema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Kojani, Hassan Hamad Omar, aliyetaka kujua mikakati ya wizara katika kutoa ajira kwa wakunga.

Naibu waziri huyo alisema ajira 55, zimetolewa kwa upande wa Pemba kwa wauguzi na wakunga katika kutekeleza majukumu yao ya kutoa huduma kwa akinamama wajawazito na watoto.

Aidha, alisema ajira 45 zimetolewa kwa upande wa Unguja ambapo lengo lake kubwa kupunguza vifo vya akinamama na watoto na kuwawezesha wanawake kujifunguwa katika vituo vya afya.

"Mheshimiwa Spika napenda kulijulisha baraza la wawakilishi kwamba Wizara ya afya tayari tumetoa ajira 100 kwa wauguzi na wakunga Unguja na Pemba ambapo lengo kuboresha huduma zetu kwenda na mikakati na malengo ya kimataifa ya kupunguza vifo vya kinamama na watoto," alisema.

Hafidh, alisema ajira zingine zinatarajiwa kutolewa ambazo zitahakikisha madaktari, wauguzi na wakunga zaidi wanaajiriwa kutoa huduma katika maeneo ya visiwa vidogo vidogo vilivyoko Unguja na Pemba.

Alisema kuna uhaba wa madaktari, wauguzi na wakunga katika maeneo ya visiwa vidogo vidogo wanavyoishi wananchi na kwamba ufumbuzi wa tatizo hilo unatarajiwa kupatikana hivi karibuni.

Pia alisema, ajira za madaktari na wakunga zitakwenda sambamba na ujenzi wa nyumba za madaktari na wasaidizi wao katika maeneo ya vijijini ikiwamo katika visiwa vidogo vidogo Unguja na Pemba.

"Vibali ya nafasi za ajira kwa madaktari, wauguzi na wakunga bado vipo. Katika awamu ya pili, tumejipanga zaidi kuvifikia vituo vya afya vilivyoko katika visiwa vidogo vidogo Unguja na Pemba," alisema.



**GIGY**

UKURASA 12

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI SEPTEMBA 10, 2022



# UMUNYANA SHANITAH Miss Rwanda anayesubiri gari kutoka Tanzania

MREMBO kutoka nchini Rwanda, amejikuta katika kigugumizi kizito baada ya kudai gari alilotakiwa kukabidhiwa kama zawadi ya mshindi halijamfikia.

Shindabno hilo lilifanyika mwaka jana katika ukumbi wa Mlimani City, Umunyana Shanitah, alishinda zawadi ya gari.


Hata hivyo, mwenyewe ametoa malalamiko ambayo yamesambaa kwa kasi katika mitandao ya kijamii kwamba gari hilo halijamfikia licha ya kuahidiwa kuletewa nchini mwake.

Baadhi ya wananchi wa nchi hiyo wameonekana wakishinikiza serikali yao kuingilia kati baada ya mshindi huyo kusisitiza katika mahojiano mbalimbali aliyofanya kwamba hajapata zawadi yake.

Kutokana na utata huo, watu walioguswa na mkasa huo wametaka mamlaka inayosimamia mashindano ya aina hiyo kuwa makini kama kweli kumejitokeza hali hiyo, kwani inaweza kuondoa imani ya washiriki.

BASI SAWA

## Gigy Money hategemei mambo mengine



MWanamuziki wa Bongo Fleva, Gigy Money, amewasihi wanawake wenzake kufanya kazi kwa ajili ya kupata manufaa yao, badala ya kuegemea kupata pesa katika mambo mengine.

Gigy Money amesema hayo wakati akitambulisha gari lake jipya aina ya V8, na kuongeza kwamba gari hilo litamrahisishia kazi zake za muziki.

"Mambo mengine yanaweza kukupa pesa, lakini kwangu pesa si tatizo nimepewa na wenye zao na kufanya kazi kwa nguvu," amesema Gigy Money.


## Barakah kawashtua wengi



MWANAMUZIKI mkongwe Baraka the Prince, amewashtua mashabiki zake baada ya kueleza kwa sasa anajipatia kipato kwa kutumbuiza katika harusi.

Kauli hiyo inaonekana na watu wengi kwamba kama ameshuka kimuziki na kwamba kilichobaki kwake ni kuangalia namna ya kujiinua au kufanya inshu zingine nje ya muziki.

Mitandao ya kijamii imejikuta ikimjadili mwanamuziki huyo, huku baadhi ya wapenzi wa muziki wakisema hatua hiyo aliyofikia Barakah ni sawa na kupotea kimuziki na si suala la kujivunia.




## ZABRON SINGERS WATAZAMA 'BAADA YA NDOA'

KUTOKA mkoani Shinyanga, kundi la Zabron Singers, wameendelea kuweka rekodi mbalimbali kwenye chati za muziki na ujio wao mpya, Baada ya Ndoa.

Kiongozi wa Zabron Singers, Japhet Zabron amesema wimbo huo ni mwendelezo wa nyimbo nzuri kwaajili ya matukio ya harusi baada ya Sweetie Sweetie kufanya vizuri.

"Tuliahidi kwamba tuna nyimbo mpya kwaajili ya harusi, tayari tumeachia Baada ya Ndoa ambao ndani ya muda mfupi umeingia kwenye 'Trend' na umewagusa watu wengi," amesema Japhet.

# Lofa: bora maskini huru

**Na Adam Fungamwango**

BORA uwe masikini huru kuliko kuwa tajiri mtumwa. Ni msemo wa tangu enzi na enzi unaoonyesha kuwa binadamu siku zote ni afadhali kuwa huru akijindesha mambo yake mwenyewe, kuliko kuwa na mali lakini ina masharti kibao.

Filamu imechezwa na Emmanuel Mkango, Ishaka Ramadhani, Sonia Barnaba, Anna Ngereja, Abdallah Mtepa, Rither Paschal na wengine wengi.

Inaanza kwa kuonyesha kuwa Mkango ana mpenzi wake aitwaye Sonia. Ni wapenzi wa kuibana tu, lakini siku moja kaka yake Sonia anawafuma nyumbani kwao na anakwenda kumwita mtu wa kuwafungisha ndoa ya mkeka.

Hata hivyo, Mkango hana kazi wala pa kukaa, hivyo ilibidi wakae nyumbani kwa mke.

Mke mwenyewe anaishi kwa bibi yake ambaye ndiye aliyemlea tangu yuko mdogo.

Mkango, anaanza kupata joto ya jiwe kutoka kwa bibi wa mkewe kutokana na kutokuwa na kazi wala kuweza kumtunza mwanamke.

Akufukuzae hakwambii toka, mambo yalianza kubadilika, hivyo Mkango akaomba ushauri kwa rafiki yake Ishaka.



Akamwambia cha kufanya ondoke ukweni. Akafanya hivyo. Huko ndiyo ikawa balaa kabisa. Nyumba za kupanga watu wengi hasa uswahilini zina mambo. Akinamama wa mjini wakamshawishi Sonia kuingia kwenye mikopo.

Kutokana na maisha duni wanayoishi, Sonia alikopa, lakini kama ilivyo kawaida kwa akinamama wengi wa uswazi, akashindwa kurudisha mkopo aliochukua.

Awali hakutaka mumewe ajue, lakini kutokana na kushindwa kurudisha rejesho, habari zikamfikia mumewe. na hii ni kwa sababu vitu vya ndani vilitaka kupigwa mnada.

Mkango akakubali kulipa. Hata hivyo siku zikapita na hakushindwa kulipa. Jamaa akaja kusomba kila kitu ndani. Hii ilimkera sana Mkango akamtimua mkewe Sonia. Akarudi nyumbani kwao.

Huku nyuma Mkango alijitahidi kutaka kuanza maisha mapya bila Sonia. Hakuweza. Alishinda kufanya chochote bila yeye.

Akaenda nyumbani kwao. Akamkuta yupo na bibi yake, pamoja na kaka aliyemfungisha ndoa ya mkeka. Akaanza kujieleza jinsi ilivyokuwa mpaka akamtimua mkewe. Pamoja na hayo akaomba msamaha. Katika hali isyokuwa ya kawaida bibi naye akamsamehe. Akamshauri kwanza arudi pale pale wakae kwenye chumba kile cha mwanzo hadi atakapopata kazi.






## Burudani za kibabe kuanza tena

BURUDANI za kibabe hatimaye zinarudi, kufuatia baada ya vituo vya utangazaji vya East Africa radio na televisheni kwa kushirikiana na kampuni THE WORKS, kuweka wazi kwamba itandaa matamasha makubwa ya muziki.

Ushirikiano huo ambao utadumu kwa miaka miwili, itafanikisha EATV na EA Radio, kuandaa matamasha makubwa ya burudani na kukata kiu ya mashabiki ambao waliyakosa siku nyingi.

Tamasha la kwanza litafanyika jijini Dar Es Salaam katika kiwanja maarufu cha burudani kilichopo Ware House, Next Door Masaki.

## MAJINA YA UTANI YALIANZIA HAPA

**Na Adam Fungamwango**

MAJINA ya utani si jambo la ajabu kwa watu wengi maarufu duniani. Wanamuziki, wasanii na wanamichezo wengi duniani pamoja na kwamba wamekuwa na majina yao halisi, lakini wengine wamekuwa wakijulikana zaidi kwa majina yao ya utani, wakati mwingine kufunika kabisa yale halisi.

Kwa mfano, wachezaji wa soka utasikia Said Mwamba, jina la utani 'Kizota' na likawa ndilo ambalo linamtambulisha zaidi, au Mohamed Hussein, ambaye jina lake la kimichezo la utani 'Tshabalala' na anatambulika zaidi kwa jina hilo kuliko lake halisi.

Lakini mara nyingi majina ya utani hayazuki tu, badala yake kuna mahali yanaanzia. Wakati mwingine inakuwa kama mzaha tu, tayari ndiyo linakuwa jina.

Sitaki hapa kueleza jinsi Kizota na Tashabalala walivyopata majina hayo, ila leo nikajikita kuelezea jinsi yalivyopatikana majina ya utani ya wanamuziki wa dansi.

**Moshi William 'TX'**

Ukitaka kulitaja jina lake ni lazima uanze na Tx Moshi William. Huyu alikuwa ni mwimbaji maarufu na mtunzi wa bendi ya Msondo Music aliyefariki mwaka 2006 jijini Dar es Salaam.

Alipewa jina la TX, na mtangazaji wa Redio Tanzania wakati huo, marehemu Julius Nyaisanga.

Mwaka 1982, alihamia Msondo akitokea Polisi Jazz Band. Na wakati huo kuna magari wa wataalam kutoka nje ya nchi yalikuwa wakisajiliwa kwa kuanzia neno TX, halafu namba za magari kama vile TZ au T kwa sasa.

Moshi alionekana ni kama mtaalamu kutoka Polisi aliyeingia Msondo, ndipo akapachikwa jina la TX, likawa kama jina lake halisi.

**Athumani Momba 'Sauti ya Chuma'**

Alikuwa mwimbaji na bendi mbalimbali kama Vijana Jazz, Bima Lee na alifariki mwaka 2005, akiwa kwenye bendi ya Msondo Ngoma Music.

Huyu alipewa jina la 'Sauti ya Chuma' kutokana na sauti yake kuwa kali na ya juu.

Hayati Hemed Maneti ndiye aliyempa jina hilo wakati akiwa Vijana Jazz. Ni wakati wa mazoezi, alipewa wimbo mmoja auimbe. Aliuimba kwa sauti kali na ya juu, kiasi kwamba Maneti akacheka na kumwambia "Mhh punguza kidogo, maana hiyo sauti kama chuma." Kuanzia hapo akaanza kuitwa 'Sauti ya Chuma.'

**Jerry Nashon 'Dudumizi'**

Huyu alikuwa mwimbaji wa bendi za Vijana Jazz na Bima Lee. Alifariki mwaka 1995. Alikuwa na sauti nzito na yenye kitetemeshi. Awali alipojiunga na Vijana kutoka Magereza Jazz alikuwa akipiga 'gitaa la rhythm.' Wakiwa safariki Maneti, alipatwa mafua, hivyo akataka msaidizi wa kuitikia, kwani asingeweza kuimbisha na kuitikia, hivyo alimtaka mmoja amsaidie. Kwa sababu Nashon aliweza, alimsaidia. Jinsi alivyoimba, ilimpendeza sana Maneti akamwambia "Wewe unaimba kama Dudumizi." Kuanzia hapo jina lake likawa Dudumizi, na ndipo rasmi alipoanza kuimba na kutunga hadi anafariki dunia.


**Rogart Hega 'Katapila'**

Labda watu wanaweza wakadhani kuwa hilo lilitokana na mambo ya muziki, la hasha. Ni kwamba kwenye miaka ya '90 wakati Hega alianza muziki akiwa na bendi za Washirika Tanzania Stars kulikuwa na viatu aina ya 'caterpillar' ambavyo vilikuwa ndiyo vinaingia nchini. Mwanamuziki huyo alikuwa mpenzi mkubwa wa kuvaa mdundo huo, kiasi cha wenzake kumpachika jina hilo.

**Mohamed Salum 'Gotagota'**

Alikuwa mwimbaji wa bendi za Tabora Jazz, Mwenge Jazz na hatimaye Vijana Jazz. Alifariki katikati ya miaka ya 1990.

Kutokana na sauti yake kuwa tamu, mashabiki waliifananisha na ndege anayegonga kwenye miti, aitwaye 'gotagota'.



# Kanye kumbe ndivyo ulivyo

RAPA wa Marekani Kanye West, amefichua jinsi uraibu wake wa kupenda filamu za ngono ulivyoharibu familia yake.

Mwanamuziki huyo bilionea kupitia ukurasa wake wa Instagram, amesema anakabiliana na ulevi huo ambao chanzo chake ni anasa za Holluwood.

Amemshutuku mama mkwe wake Kris Jenner, kwa kuwapeleka binti zake Kim na Kylie katika jariba maarufu la playboy ambalo analiona kama danguro la ngono.



## Okoye sheria ni msumeno

STAA wa muziki kutoka Nigeria, Paul Okoye, ameingia kwenye orodha ya Wanigeria wanaoshutumu kuhusu kukamatwa kwa rapa, Ice Prince.

Katika chapisho aliloweka katika ukurasa wake wa Instagram amesema ikiwa afisa wa polisi ataingia kwenye gari lake na kumwambia aendeshe, hatokubali kufanywa kama ametekwa nyara.

Maoni ya Okoye yanajiri siku chache baada ya Ice Prince, kukamatwa kwa madai ya kushambulia afisa wa polisi jijini Lagos.

## Nicolas, Riko wapata mtoto

MWIGIZAJI mkongwe wa filamu nchini Marekani, Nicolas Cage na mkewe Riko Shibata, wamepata mtoto wao wa kwanza wa kike.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Cage amewaambia mashabiki zake kwamba yeye na mkewe wana furaha kutokana na zawadi ya mtoto wa kike waliyopewa na Mungu.

"Nicolas na Riko tuna furaha kuwajulisha kuzaliwa kwa mtoto wetu wa kwanza wa kike , mama yake ana afya njema," ameandika cage.






## Eniola jipe raha mwenyewe

MSANII wa filamu wa kike kutoka Nigeria, Eniola Badmus, amefanya kufuru baada ya kujinunulia gari la kifahari aina ya Mercedes Benz, katika siku yake ya kuzaliwa.

Badmus ametumia ukurasa wake wa Instagram kuliweka wazi gari hilo, huku akiambatanisha na ujumbe unaoeleza furaha yake ya kupata gari hilo.

"Ni zawadi ya siku yangu ya kuzaliwa, ukweli sijui nilipoanzia lakini najaribu, hii inatokana na kufanya kazi kwa nguvu," ameandika.

## Odoputa amlilia baba yake

STAA wa filamu za Nollywood Uche Odoputa, bado anaendelea kuwa na majonzi baada ya baba yake Kenneth Odoputa, kutimiza miezi minne akiwa mikononi mwa watekaji nyara.

Odoputa, ameandika kwenye ukurasa wake wa Instagram kwamba amekuwa na wakati mgumu kujua baba yake wapi aliko baada ya watu wasiojulikana kumteka nyara na kumpeleka sehemu isiyojulikana.

"Inasikitisha sana na inahuzunisha jimbo langu la Imo linavyopoteza watu zaidi kuliko wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe, akiwemo baba yangu Kenneth Odoputa ambaye amechukua kwa miezi 4 sasa bila taarifa yoyote," ameandika.



MAKALA

# Utafiti TWAWEZA unapobaini unafuu upatikanaji maji Dar

Na Joseph Mwendapole



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) Mhandisi Cyprian Luhemeja, akitoa maelezo kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Amos Makalla na wa Pwani Abubakari Kunenge, kuhusu namna uzalishaji wa maji katika mtambo wa Ruvu Juu unavyofanyika chini ya usimamizi wa DAWASA

HUDUMA ya maji ni mojawapo ya hitaji muhimu la kila siku kwa kila mwanadamu kwa kuwa maji hutumika kwa matumizi mbalimbali hususani majumbani na viwandani kwa shughuli za kiuchumi.

Dar es Salaam ni mojawapo ya majiji yanayokua kwa kasi kiuchumi katika Bara la Afrika, huku likiwa na idadi kubwa ya watu na kuchochea uhitaji mkubwa wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira.

Katika kuhakikisha maji yanapatikana kwa uhakika, serikali kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imekuwa ikifanya uwekezaji mkubwa wa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya majisafi kwa lengo la kuhakikisha huduma hiyo kwenye miji inapatikana kwa asilimia 95 na vijijini kwa asilimia 85.

Moja ya kipaumbele kikuu cha Mamlaka ni kuhakikisha huduma ya majisafi kwa Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani inaimarika na kufikia asilimia 100 ifikapo mwaka 2023.

Upatikanaji wake kwa sasa kwa Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani umefikia asilimia 96 kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali iliyotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2021/22 na kufanikiwa kuongeza upatikanaji wa huduma kwa wakazi.

Katika kutekeleza azma ya serikali ya kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji mijini kwa asilimia 95 na asilimia 85 vijijini, DAWASA iliwekeza asilimia 35 ya mapato yake ya ndani kutekeleza miradi mikubwa ya majisafi.

Miongoni mwa miradi hiyo ni ule wa Gongo la Mboto uliogharimu bilioni 7.6, mradi wa maji Kibamba - Kisarawe uliogharimu bilioni 10, mradi wa maji Jet - Buza awamu ya kwanza uliogharimu bilioni 2.2 na mradi wa maji Mlandizi - Chalinze - Mboga uliogharimu bilioni 18,

Miradi mingine ni Zegereni, mradi wa kusambaza maji Makongo hadi Bagamoyo unaogharimu bilioni 65.4, pamoja na miradi ya maji ya kijamii inayotekelezwa kwa lengo la kuwapatia maji wakazi walio nje ya mtandao rasmi wa DAWASA.

Hatua hii ya utoaji wa huduma kwa asilimia 96 kwa sasa imefikiwa kupitia jitihada mbalimbali zilizowekwa na DAWASA ikiwemo utekelezaji wa miradi mikubwa na ya kimkakati iliyowezesha uboreshaji wa huduma na kuongeza upatikanaji wa huduma kwa kila mwananchi.

Kwa mwaka wa fedha 2022/23, DAWASA imejiwekea mipango mbalimbali ya kuboresha na kuhakikisha huduma ya majisafi inapatikana kwa wananchi wote kwa asilimia 100 na kwa ubora zaidi kufikia mwaka 2023.

Kwa mujibu wa ripoti ya hali ya upatikanaji wa huduma za kijamii kitafiti iliyotolewa na Taasisi ya Twaweza ya mwaka 2022, inaonesha kuwa hali ya upatikanaji wa maji kwa Dar es Salaam imeimarika kwa asilimia 17 kulingana na idadi ya wananchi waliohojiwa kwenye utafiti.

Akiwasilisha ripoti hiyo jijini Dar es Salaam Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Twaweza Aidan Eyakuze amesema kuwa katika utafiti walioufanya mwaka 2022 kutoka kwa wananchi waliohojiwa umeonesha huduma ya majisafi kuimarika kwenye maeneo mengi ya jiji la Dar es Salaam.

Ripoti imeeleza pia kuwa kati ya mambo makuu matatu ambayo wananchi wamependekeza kwa Serikali kuipa kipaumbele ni huduma ya majisafi kwa kuimarisha upatikanaji wake kwa wananchi.

Ameeleza kuwa taarifa zilichukuliwa kutoka kwa wananchi 3,000 waliohojiwa mwezi Oktoba na Novemba 2021, na pia katika mwezi Juni na Julai mwaka 2022.

Kupitia utafiti huu, maoni yaliyokusanywa kutoka kwa wananchi kuhusu huduma ipi ambayo wananchi wangependa kuona Serikali inaipa kipaumbele ni pamoja na upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa Dar es Salaam na Pwani.

Utafiti umeonesha pia kuwa, kwa wananchi waliohojiwa kuhusu matatizo makuu wanayoyaona kwenye maeneo yao, wananchi walibainisha kuwa upatikanaji wa maji kwa jiji la Dar es Salaam kwa kipindi cha mwezi Juni mpaka Julai mwaka 2022 ni wa hali nzuri na huduma haijawa na shida ya uhaba wa maji.

Utafiti umeonesha pia kuwa hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa Dar es Salaam umeendelea kuimarika ambapo kwa mwaka 2021 uhakika wa upatikanaji wa majisafi umeongezeka kwa asilimia 16 na kwa mwaka 2022 upatikanaji wa huduma hiyo umeongezeka kwa asilimia 17 kulingana na idadi ya wananchi waliohojiwa.

Utafiti huu unadhihirisha mafanikio chanya ambayo yamepatikana katika utoaji wa huduma ya majisafi kwa Dar es Salaam kupitia mikakati bora iliyowekwa na kutekelezwa na serikali kupitia DAWASA mpaka kufikia mwaka wa fedha 2021.

Mbali na hapo utafiti wa Twaweza umebainisha kuwa mbali na changamoto nyingine zilizoorodheshwa na wananchi kama kupanda kwa gharama ya maisha, lakini upatikanaji wa huduma ya majisafi haujabainishwa kuwa changamoto kwa eneo lote la Dar es Salaam.

Katika utafiti huo, wananchi waliohojiwa kwa kipindi cha mwezi Juni na Julai 2022 walisema kuwa kati ya huduma muhimu ambayo wanapendekeza Rais Samia Suluhu Hassan kuzipa kipaumbele ni pamoja na uboreshwaji wa huduma ya majisafi.

Akielezea mipango iliyopo ya uboreshaji na ukuzaji wa huduma kwa mwaka wa fedha 2022/23, Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA Mhandisi Cyprian Luhemeja, amesema kupitia mpango biashara wa Mamlaka wa miaka mitano 2022/23 - 2024/25, Mamlaka imejipanga kikamilifu kwa kutenga bajeti ya Trilioni 1.16 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya majisafi kwa lengo la kuhakikisha huduma inapatikana kwa asilimia 100 ifikapo mwaka 2023.

Mamlaka imeainisha mikakati ya muda mfupi na muda mrefu ya kuhakikisha huduma ya majisafi inapatikana muda wote, ambapo kwa mpango wa muda mfupi Mamlaka imejenga mabwawa ya muda mfupi kwenye chanzo cha maji cha Ruvu chini ambayo yatahifadhi maji yatakayotumika wakati wa uhaba wa mvua kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

"Wakati kwa mipango ya muda mrefu, Mamlaka inakusudia kuanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa ujenzi wa Bwawa la kuhifadhi maji la Kidunda kazi inayotarajiwa kuanza kutekelezwa mwezi mwezi Oktoba mwaka 2022," anasema.

Pia Mhandisi Luhemeja amesema kuwa Mamlaka inatekeleza mradi wa maji

Mshikamano unaolenga kuondoa shida ya maji kwa wakazi wa Mbezi, Kwembe na maeneo ya Kibamba, mradi unagharimu bilioni 4.8 ambazo ni fedha za ndani na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba.

"Mamlaka imeanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa vituo vya umma ambapo vituo 30 vinajengwa kwenye Halmashauri zote tano za Dar es salaam kwa gharama ya shilingi bilioni 3.3, pia ujenzi wa mitandao midogo ya uondoshwaji majitaka kutoka majumbani kwa wananchi walioko pembezoni na wenye kipato cha chini," ameeleza Mhandisi Luhemeja.

Mhandisi Luhemeja amebainisha kuwa katika mwaka wa fedha 2022/23, Mamlaka imejipanga kuongeza utoaji wa huduma kupitia magari ya uondoshwaji majitaka ambapo shilingi bilioni 1.2 zitatumika kununua magari mengine ili huduma ya majitaka ifike kwa wananchi wote.

Kwa utafiti huu wa Twaweza imeipongeza Serikali kupitia DAWASA kwa jitihada zote zilizosababisha kufikisha asilimia 96 ya upatikanaji wa huduma.

Imetoa rai kwa uwepo wa uharaka wa utekelezaji wa miradi ya kimkakati iliyobainishwa kufikisha asilimia 100 ya upatikanaji huduma kulingana na mpango biashara wa mamlaka wa miaka mitano ili Serikali iweke nguvu zaidi eneo la Vijijini.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Mtoto zamani anapotumwa dukani

## ●Anaimba alichotumwa njia nzima
## ●Ukimsemsha kasahau, akirudi fimbo



Na Adam Fungamwango

"SUKARI tatu, mchele tano, sigara kilo moja na kiberiti nusu..." Ni wimbo ambao unaimbwa na mtoto aliyetumwa dukani na baba, mama au mlezi wake.

Halafu hapo tayari ameshachanganya madawa mara baada ya kukutana na mtu ambaye amemsemesha, au kumsalimia na kusababisha kusahau yote aliyotumwa.

Anafika kwa dukani na kutaja vitu ambavyo ametumwa. Bahati nzuri akikutana na muuzaji ambaye anajua kuunganisha vitu anaweza kumuelewa na kumsaidia.

Hakuna kitu kinaitwa sukari tatu, halafu sigara kilo moja, mchele tano na kiberiti nusu, hapa muuzaji anachukua pesa na kuanza kuungnisha mwenyewe.

Mtoto kama huyo hawezi kutumwa bidhaa kama mchele au sukari kilo tano, na hawezi kutumwa viberiti vitano, hivyo hiyo tano inabaki kwa sigara. Hapo ni kwamba sigara tano. Anakwenda kwenye sukari ni kwamba katika mazingira ya kawaida hakuna mzazi anayeweza kumtuma mtoto kilo moja, pia ni nadra sana sukari dukani kununuliwa kilo moja na watoto au akinamama.

**Mtoto anaitwa kwanza na kuambiwa aende dukani. Anapewa maagizo ya vitu vingi ingawa ni vidogo vidogo, lakini vinavyoweza kumchanganya.**



Labda kinababa tena mwisho wa mwezi. Kwa hiyo hapo atapima sukari nusu. Anakwenda kwenye mchele, ni kwamba ile kilo moja ambayo inatajwa ni sigara, ni mchele kilo moja, halafu kinabaki kiberiti.

Muuzaji anakuwa tayari ameshajiongeza na kumpa kile kinachotakiwa na mtoto anarudi nyumbani.

Hayo ndiyo yalikuwa maisha ya watoto wa zamani.

Ni miaka ile ile ya 1990 kurudi nyuma. Ni miaka ambayo watoto walikuwa wakilelewa na wazazi wao kama wapo kwenye kambi za jeshi.

Mtoto anaitwa kwanza na kuambiwa aende dukani. Anapewa maagizo ya vitu vingi ingawa ni vidogo vidogo, lakini vinavyoweza kumchanganya.

Huyo aliyejichanganya alitumwa kununua sukari nusu, mchele kilo moja, sigara tano na kiberiti. Kwa sababu ya utundu wa watoto wa zamani wanakuwa na mambo mengi kiasi kwamba anaweza kufika njiani akacheza na wenzake, halafu akasahau kila kitu.

Wazazi wa zamani kama kawaida yao hawakumkopesha mtu, kipigo ilikuwa ni sehemu tu ya maisha, mtoto anayesahau ametumwa nini, akarudi nyumbani kuuliza ni lazima kabla ya kukumbushwa, atapata mkong'oto halafu anaambiwa tena upya na kuambiwa arudi tena dukani.

Mfano huyu aliyejichanganya, kama hakukutana na mwenyeduka muelewa na kuunganisha 'doti', akarudi nyumbani kuuliza, kipigo kilikuwa kinamsubiri.

Kwa bahati mbaya sana zamani maduka yalikuwa mbali kidogo na nyumba za watu wengi au vijiji, tofauti na sasa, hivyo iliwachukua watoto muda kufika.

Hapa njiani chochote kinaweza kutokea kikatibua mipango yote. Kutokana na hilo, baadhi sasa ya watoto wa zamani wakabuni njia ya kuimba njiani.

Anapotumwa ili asisahau, anatoka hapo na kuanza kuimba. Wimbo wenyewe ndiyo ni kutaja vitu alivyotumwa, kiasi chake na hata kama chenji inarudi pia atakariri au kukaririshwa ili asisahau.

Wakati mwingine hata wazazi wakawakaririsha watoto wao na kuongeza neno "sasa ole wako usahau".

Hiyo inakwenda mbele zaidi kwani baadhi ya wazazi kwa kujua watoto wao wamezidi utundu, wanaweza toka hapo kwa minajiri ya kwenda dukani lakini wakacheza njiani walipigwa 'mkwara' na maneno haya "natema mate, sasa yakauke uwe hujarudi."

Hapo mtoto atakimbia bila kusimama hadi dukani. Tatizo kubwa lililowafanya wasahau walichotumwa ni kusemeshwa njiani, kucheza anapokutana na watoto wenzake, au kama ametumwa vitu vingi.

Na kwa sababu dukani au gengeni kunakuwa mbali na nyumbani, basi hutumia njia mbalimbali za kufika mapema.

Wengine walitumia kuendesha magurudumu, au ringi za basikeli. Akitumwa anachukua na kuanza kukimbia nalo akilisukuma kwa mikono, na wakati mwingine kutumia mti, ili mradi tu kupata sababu ya kuwahi dukani.

Tuma meseji 0716 350534

HABARI KIMATAIFA

# HUYU NDIYE MALKIA ELIZABETH

- Amevunja rekodi ya kuongoza Uingereza
- Makubwa yatarajiwa kuagwa, kuzikwa kwake

**LONDON,** UINGEREZA

DUNIA iko katika maombolezo baada ya Malkia Elizabeth II wa Uingereza kufariki dunia siku ya Alhamisi.

Kiongozi huyo ambaye amevunja rekodi kwa kuhudumu muda mrefu zaidi nchini Uingereza, amefariki akiwa na umri wa miaka 96, na kuitawala nchi hiyo kwa miaka 70.

Malkia Elizabeth alishika kiti cha ufalme mwaka 1952 na alishuhudia mabadiliko makubwa ya kijamii.

Kutokana na kifo chake, mwanawe wa kwanza Charles, ataongoza nchi kwa maombolezo kama Mfalme mpya na mkuu wa nchi kwa milki 14 za Jumuiya ya Madola.

Katika taarifa yake, Mfalme Charles alisema "Kifo cha mama yangu mpendwa Malkia, ni wakati wa huzuni kubwa kwangu na wanafamilia wote.Tunaomboleza sana kifo cha Malkia mpendwa na Mama anayependwa sana. Najua kumpoteza ni jambo litakalosikika sana kote nchini, Milki na Jumuiya ya Madola, na kwa watu wengi duniani kote."

Katika taarifa iliyotolewa na Jumba la Buckingham ilisema Malkia alikufa kwa amani huko Balmoral mchana wa Alhamisi.

Watoto wote wa Malkia walisafiri hadi Balmoral, karibu na Aberdeen, baada ya madaktari kumweka Malkia chini ya uangalizi wa matibabu.

Mjukuu wake, Prince William, pia alikuweko akiambatana na ndugu yake Prince Harry.

Katika maisha ya Malkia Elizabeth II, alishuhudia vipindi tofauti vya mageuzi kama mabadiliko kutoka kwa himaya hadi Jumuiya ya Madola, mwisho wa Vita Baridi na kuingia kwa Uingereza na kujiondoa kutoka Umoja wa Ulaya.

Utawala wake ulihusisha mawaziri wakuu 15 kuanzia na Winston Churchill, aliyezaliwa mwaka 1874, hadi Liz Truss, aliyezaliwa miaka 101 baadaye.

Alifanya kikao cha kila wiki na waziri mkuu wake katika kipindi chote cha utawala wake.

Katika Jumba la Buckingham huko London, umati wa watu waliokuwa wakisubiri taarifa kuhusu hali ya Malkia walianza kulia waliposikia kifo chake. Bendera ya Muungano juu ya Kasri ilishushwa hadi nusu mlingoti saa 18:30 BST.

**KUZALIWA KWAKE**

Malkia Elizabeth alizaliwa Alexandra Mary Windsor, huko Mayfair, jijini London, Aprili 21 mwaka 1926.

Wachache walitabiri kwamba angekuwa malkia, lakini mnamo Desemba 1936 mjomba wake, Edward VIII, alijiondoa kwenye kiti cha ufalme na kuoa Mmarekani aliyetalikiana mara mbili, Wallis Simpson.



Malkia Elizabeth

Baba ya Elizabeth alikuwa Mfalme George VI na, akiwa na umri wa miaka 10, Lilibet, kama alivyojulikana katika familia, alikuwa mrithi wa kiti cha ufalme.

Katika muda wa miaka mitatu, Uingereza ilikuwa katika vita na Ujerumani ya Nazi. Elizabeth na dadake mdogo, Princess Margaret, walitumia muda mwingi wa vita katika jumba la Windsor Castle baada ya wazazi wao kukataa mapendekezo ya kuhamishwa hadi Canada.

Baada ya kufikisha umri wa miaka 18, Elizabeth alitumia muda wa miezi mitano kujifunza ufundi wa msingi wa wa magari na ustadi wa kuendesha.

Kupitia vita, alibadilishana barua na binamu yake wa tatu, Philip, Mkuu wa Ugiriki, ambaye alikuwa akihudumu katika Jeshi la Wanamaji la Kifalme.

Mapenzi yao yalistawi na wenzi hao walifunga ndoa huko Westminster Abbey mnamo 20 Novemba 1947, na mkuu huyo akichukua jina la Duke wa Edinburgh.

Mtoto wao wa kwanza, Charles, alizaliwa mwaka wa 1948, akifuatiwa na Princess Anne, mwaka wa 1950, Prince Andrew, mwaka wa 1960, na Prince Edward, mwaka wa 1964.

Kati yao, waliwapa wazazi wao wajukuu wanane na vitukuu 12.

Familia ya kifalme sasa imeingia katika kipindi cha maombolezo.

**MALKIA ELIZABETH ATAKAVYOAGWA**

Kifo cha Malikia Elizabeth ni hitimisho ya huduma yake ya muda mrefu zaidi katika historia ya Uingereza. Kaatika taratibu za mazishi ya kifalme, taratibu zifuatazo zitafuatwa wakati wa shughuli za kuaga na mazishi yake.

Ukumbi wa Westminister

Baada ya jeneza lake kurudi mjini London, mwili wa Malkia utalazwa katika ukumbi wa Westminister kwa takriban siku nne kabla ya mazishi yake.

Hapo itawapa ruhusa raia wa Uingereza kuutazama mwili wake na kuuaga.

Ukumbi huo ndio wa zamani zaidi ikilinganishwa na kumbi nyingine Westminister. Katikati ya serikali ya Uingereza. mtu wa mwisho wa familia ya Ufalme kuwekwa katika hali hiyo alikuwa mama yake Malkia mwaka 2002.

Jeneza la Malkia litawekwa katika eneo la juu, linalojulikana kama Catafalque, chini ya dari lililojengwa na mbao. Kila kona ya eneo hilo litalindwa na wanajeshi kutoka vitengo vyake ambao wanahudumia familia ya Kifalme.

Mwili utasafirishwa hadi katika ukumbi wa Westminister kutoka Kasri la Buckingham kwenye msafara utakaokuwa ukiendeshwa polepole wakiambatana na gwaride la kijeshi la familia ya Kifalme.

Watu wataweza kuutazama msafara huo wakati ukipita barabarani kupitia skrini kubwa zinazotarajiwa kuwekwa katika bustani za kifalme.

Jeneza lake litafunikwa kifalme na litakapowasili Westminister litawekewa taji la Kifalme orb na fimbo.

Mara tu jeneza hilo litakapowekwa ndani ya ukumbi huo, ibada fupi itafanyika. Baadaye raia wataruhusiwa kuingia.

Mazishi ya Malkia yanafanyika lini?

Mazishi ya Serikali ya Malkia yanatarajiwa kufanyika huko Westminster Abbey chini ya wiki mbili zijazo. Siku kamili itathibitishwa na Kasri la Buckingham.

Abbey ni kanisa la kihistoria ambako wafalme na malkia wa Uingereza wanatawazwa, ikiwa ni pamoja na alipotawazwa Malkia Elizabeth mwaka 1953, na alipokula kiapo cha ndoa na Prince Philip mwaka 1947.

Hakujakuwa na ibada ya mazishi ya mfalme katika kanisa la Abbey tangu Karne ya 18, ingawa mazishi ya mama yake Malkia yalifanyika huko mnamo 2002.

Siku itaanza kwa jeneza la Malkia kubebwa kutoka Ukumbi wa Westminster hadi eneo la Westminster Abbey kwenye Gari la Jeshi la Wanamaji la Kifalme.

Gari hilo lilionekana mara ya mwisho mnamo 1979 katika mazishi ya mjomba wake Mwanamfalme Philip, Lord Mountbatten, likiwa na mabaharia 142 kutoka Jeshi la Wanamaji la Kifalme.

Wajumbe wakuu wa Familia ya Kifalme, pamoja na Mfalme mpya, wana uwezekano wa kuambatana na msafara huo.

Ibada hiyo huenda ikaendeshwa na Dean wa Westminster David Hoyle, huku Askofu Mkuu wa Canterbury Justin Welby akitoa mahubiri. Waziri Mkuu Liz Truss anaweza kuitwa kutoa hutuba.


Baada ya ibada ya mazishi, jeneza la Malkia litatolewa katika msafara kutoka Westminster Abbey hadi Wellington Arch, kwenye bustani ya Hyde Park Corner ya London kabla ya kuelekea Windsor kupitia gari la kubeba maiti.

Jeneza la Malkia litafanya safari yake ya mwisho alasiri hiyo hadi St George's Chapel katika kasri la Windsor.

Mfalme na washiriki wakuu wa Familia ya Kifalme wanatarajiwa kujumuika na msafara katika Quadrangle ndani ya Kasri la Windsor kabla ya jeneza kuingia kanisa la Mt. George Chapel kwa ibada.

Mt. George Chapel ni kanisa linalochaguliwa mara kwa mara na familia ya Kifalme kwa ajili ya harusi, ibada za kawaida na mazishi. Ni mahali ambako Duke na Duchess wa Sussex, Prince Harry na Meghan, walifunga ndoa na ambapo mazishi ya marehemu mume wa Malkia Prince Philip yalifanyika pia.

Jeneza la Malkia litashushwa ndani ya Jumba la Royal Vault kabla ya kuzikwa katika kanisa la ukumbusho la King George VI, lililoko ndani ya St George's Chapel.




Barabara kutoka ukumbi wa Westminister Abbey

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**DEBORA SHEKYA MAKERE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4900/0008** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MKUZA GIRLS SEKONDARI mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya **Polisi: DSM/PHQ/RB/356021/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHN GELEFASI KACHECHE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 298 BKR – MITSUBISHI FUSO.** Chassis namba: **FK618K5223611.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /4342/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MAISAM MOHAMED FAZAL** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 786 BED – TOYOTA LANDCRUISER.** Chassis namba: **HDJ810054978.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /4896/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VALENCE HONORARUSTURUKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 390 AAX – LANDROVER DEFENDER.** Chassis namba: **SALLDHMFTHA902938.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /4893/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KASSIM ZUBERI NGWAHE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 577 CJU– SUZUKI CARRY.** Chassis namba: **DD51T360046.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /4895/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAID SAID MWIKONI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 803 ALM – HINO FD3HKA.** Chassis namba: **FD3HKA10427.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /4894/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARYAM MOHAMED SALIM** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 203 AGZ – HONDA CG250.** Chassis namba: **MD03E1024858.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /4897/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HAMISI SADI KANGAULAYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 301 DDF – FAW TRACTOR HEAD.** Chassis namba: **LFWSVXPJ7EAD20975.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /4290/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HAMISI SADI KANGAULAYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 199 DDE – FAW CA3320.** Chassis namba: **LFNKVXPJ2EAD22007.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /4290/2022.**

## 30 Ton Coles Crane with 112 Feet boom and 145 feet extension.

Crane is in working condition but need some repair to put it in best shape. Going cheap only for 32 million based (exclusive VAT) on as it is where it is.

**Please contact: 0687 512244.**

**RAIBA LOGISTICS TANZANIA LIMITED**
**(COMPANY NUMBER 138585824)**
**In member's Voluntary Liquidation**

**Notice of Final Meeting and Dissolution of the Company.**
**(Under section 355 of the Companies Act, 2002)**

**Call for Final Meeting and Dissolution of the Company.**

The Liquidator intends to convene a general meeting of the company on 10/10/2022. Given circumstances, the meeting will only be held virtually. That is, no physical meeting will be available.

The main purpose of the proposed meeting is to lay before the members an account showing how the winding up has been conducted and the property of the company, if any, has been disposed of. The proposed meeting shall take place virtually on 10/10/2022 at 3pm EAT.

In case of any query pertaining to the said meeting kindly send them to the liquidator's email via **pascal@audaadvocates.com or mshanga3@gmail.com.**

.................................
**Pascal Mshanga, advocate**
**The Liquidator**
**For and on behalf of**
**Raiba Logistics Tanzania Limited**
**(In member's Voluntary Liquidation)**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 96 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late:**
**LOTH SIKWESE MULUNGU**

**BY 1. JAPHET LOTH MULUNGU**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the **25day of SEPTEMBER.........2022**

**Dated at MOROGO this 8 day of SEPTEMBER.........2022**

.................................
RESIDENT MAGISTRATE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
P.O. Box 560, Morogoro

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ALEX SHUSHU NYANDA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA SUNLG YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 565 CFB.** ENGINE NO **SL157FMI18939226** NA CHASSIS **LBSPJB5XJ9028979.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **GEI /MBO/RB/ 206481 /2022.**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-22

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Wakati akiwaza yaliyoandikwa, mlango uligongwa na Bakari aliingia.

Siwatu hakutaka kabisa Bakari ajue kama alikuwa anasoma barua. Akajua kama akigundua ni ya huyo mwanaume aliyemtolea mahari, anaweza kukasirika.

Akataka kuificha karatasi ile. Bakari aliona. Hakuonyesha hisia yoyote kama kuna kitu anataka kufanya. Akamsogelea. Ghafla akamnyang'anya. Siwatu alishtuka, lakini hakuwa na la kufanya.

"Nataka nimsome huyu mjinga anasemaje?" Siwatu alikaa pembeni akiwa na wasiwasi mkubwa juu ya tukio hilo.

Bakari alisoma kila kitu, akamaliza. Cha ajabu, alichokuwa anafikiria Siwatu siyo kilichotokea.

Akidhani atakasairika kutokana na barua hiyo, badala yake akatabasamu.

"Ndicho ulichokuwa unasoma hiki?" Akauliza huku akitabasamu. Siwatu hakujibu, kwani hakujua kama ni tabasamu halisi au la bandia.

"Jamaa ni mwandishi mzuri sana huyu. Hata mimi kanifurahisha. Sasa kama anajifanya anatumia umahiri wake wa kuandika kukushawishi wewe, mimi nitatumia mdomo."

Bado Siwatu alikuwa njia panda. Hakuelewa Bakari alikuwa anataka kufanya nini.

"Hii stori yake sijui ya ukweli au ya uongo, mimi nitakuelezea yangu kwa mdomo."

"Unafanyaje? Mbona una masihara sana Bakari ?"

"Na mimi nina yangu, ila yeye kaandika, mimi nitakuhadithia kwa mdomo."

"Hadi anakuja hapa saa 12:00 jioni nitakuwa nimeshamaliza. Na yeye nitakuwa nishammaliza kabisa."

"Bakari kuna vitu vingine siyo vya masihara bwana, kwani, yeye si kaleta tu karatasi kwani ndiyo nimesema amefanikiwa?"

"Hapana, huyu amedhamiria, na nikifanya masihara hapa nitatoka kapa. Naona kabisa dalili za kukukosa. Hebu njoo hapa tukae nikupe ya kwangu halafu upime mwenyewe stori ili ni nzuri zaidi ya nyingine."

. Na yeye nitakuwa nishammaliza kabisa."




**"Usiwe unasimulia kisa hicho, huwa unanipa simanzi sana mpenzi wangu." Bakari alifarijika mno kuitwa mpenzi.**

Bado Siwatu alikuwa hajamuelewa au kujua nia ya Bakari ni nini. Hata hivyo moyo ulitulia baada ya kuona hajakasirika kumkuta na barua ile, na hata baada ya kuisoma.

"Na mimi ni nilikwambia kuwa nilitekwa kule nyuma?"

Siwatu aitikia kwa kichwa.

"Mimi nilipelekwa hadi sehemu moja hivi wala siifahamu nikaambiwa nisimamame,, nikamsikia mmoja akiuliza kama wamtwange risasi au la.

Yule mkubwa wao akasema nisipigwe risasi kwa sababu watashtua watu kwa kuwa pori lipo karibu na watu. Nikamsikia akisema mpigeni tu kisawasawa hadi afe hapo hapo porini, ama askari wachukue siku nyingi kabla ya kuikuta maiti, au iliwe na wanyama wakali na isionekane tena.

Baadaye yule yule mkuu wao akawaambia basi atammaliza mwenyewe, wao watangulie kwenye gari yeye atakuja baadaye."

"We Bakari umechanganyikiwa?" Siwatu akauliza.

"Kwa nini?"

"Hicho unachokiongea?"

"Kwani mimi na wewe tumejuana vipi?"

"Kwa sababu ya kukuokota ukiwa umetupwa porini."

"Hapa kwenu si ndiyo?"

"Ndiyo, sasa unaona ajabu vipi?"

"Mimi naona kama unaendelezea huyu aliyeniandikia barua. halafu unafanya utani."

"Hapana huyo ya kwake, na mimi ya kwangu, inawezekana zinafanana, lakini kila mtu na lake. Yeye kamalizia hapo, mimi naendelea."

"Hata endelea." Siwatu alitaka kuendelea kusikia mzaha wa Bakari.

"Nadhani yule mtu aliyeniacha hakufanya kwa bahati mbaya, ni makusudi. Kwa sababu nia ilikuwa nipigwe risasi, akakataa, akataka nife niliwe na wanyama, baada ya kunipiga sana, akawaambia waache, ili animalize mwenyewe, akawaambia waende kwenye gari. Akanifuata tena alikuwa na bastola, lakini hakupiga. Akaniangalia tu, halafu akaondoka na kuaashiria wenzake kuwa huyu mtu amekufa. Ukweli lile tukio lilikuwa kama ndoto kwani nguvu zilikuwa zinanitoka taratibu na nikazirai."

"Umemaliza?"

"Bado ndiyo nakuja hivyo."

"Mwanaume una tabu wewe."

"Basi, ile nafumbua macho nakutana na wasichana watatu wananiangalia. Hata kuangalia ilikuwa tabu sana, macho hayakuwa na nuru na nilikuwa niko hoi kwa kipigo. Nilikuwa nataka kuwapa ishara ya kwamba wasiondoke wanisaidie, lakini mikono na kila kitu kilishindwa kufanya kazi. Nikaona kabisa kama wakiondoka na kuniacha nikakaa siku nzima nitakufa kwa kutokwa na damu nyingi, ukosefu wa matibabu, njaa na kiu.

Kwa bahati mbaya waliondoka, nikajihesabu sasa mimi ni mfu, nilishaanza kusali ili Mwenyezi Mungu aniweke mahali pema peponi nilifika, nikaanza kutubu na dhambi zangu. Saa moja baadaye akaja msichana mmoja. Ni msichana wa ajabu, sijui ilikuwaje akaachana na wenzake akaja na ndoo yake ya maji. Akaninywesha, akanimwagia maji nikapata nguvu. Akaniambia anakwenda kijiji kuita watu waje kunisaidia. Nilimsikia kwa mbali, lakini sikuweza kumjibu. Na kweli baadaye akaja na vijana wawili kuniokoa. Hadi leo imebaki hadithi ya kusimulia wajukuu zangu nikibahatika kufikia uzee na Mungu akinipa uzazi..."

"Basi basi usiendelee..." Ilikuwa ni sauti ya Siwatu. Hapo sasa alishajua kuwa huko mwisho huyo hao wasichana watatu mmoja ni yeye, na na aliyekuja baadaye na kumfanyia hayo yote ni yeye. Ndicho alichokifanya siku ile alipoiona sura yake mara ya kwanza. Na ndicho kisa cha kukutana, akaishi kwao kwa miezi mitatu kabla ya kuondoka.

"Usiwe unasimulia kisa hicho, huwa unanipa simanzi sana mpenzi wangu." Bakari alifarijika mno kuitwa mpenzi.

"Hapana nimesimulia na mimi baada ya mleta barua kusimulia ya kwake, sasa utapima mwenyewe nani zaidi. Aliyeandika au aliyesimulia. Aliyeandika kaandika vizuri zaidi na aliyesimulia, hadi mwenyewe machozi yanakulenga..."

Sauti za hodi zikasikika. Hazikuwa ngeni. Ni Dibwela kaka yake Siwatu, Dibwela na Billy.

Walipoingia Siwatu bado aliendelea kushangaa kwa sababu aliambiwa kuwa ndiyo muda ambao mchumba wake atawasili. Ilikuwa ni saa 12:00 jioni.

Hilo lilimpa faraja kwa mbali Siwatu, na kuona sasa anaweza kughairi kuolewa na mtu huyo, badala yake kwa mtu anayempenda Bakari.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# RUFA ATUA SIMBA QUEENS, KUWAVAA WENYEJI ASFAR

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba Queens imekamilisha usajili wa golikipa, Mkenya, Caroline Rufa, kwa ajili ya kuongeza nguvu kuelekea fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake zitakazofanyika baadaye mwaka huu, wawakilishi hao wa Afrika Mashariki na Kati wamepangwa Kundi A na wenyeji ASFAR ya Morocco.

Timu nyingine zilizoko katika kundi hilo ni pamoja na Green Buffaloes ya Zambia na Determine Girls kutoka Liberia.

Rufa, amesaini mkataba wa miaka miwili kuitumikia Simba Queens akitokea Fountain Gate Princess ya jijini, Dodoma ambayo inashiriki Ligi Kuu ya wanawake Tanzania.

Mkenya huyo ataungana na magolikipa wengine waliokuwa katika kikosi hicho ambao ni Zubeda Mgunda na Gelwa Yonah, kipa bora wa michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Ukanda wa CECAFA iliyomalizika hivi karibuni.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Meneja wa Simba Queens, Selemani Makanya, alisema usajili wa nyota huyo umefanyika kutokana na mapendekezo ya benchi la ufundi ambalo lina malengo ya kwenda kufanya vizuri kwenye fainali hizo za Afrika ambazo zitachezwa nchini Morocco.

Makanya alisema usajili wa kipa huyo haumaanishi walinda milango waliopo si wazuri, lakini umedhamiria kuimarisha na kuongeza nguvu katika nafasi hiyo muhimu katika timu yao.

"Caroline Rufa, ni mchezaji halali wa Simba Queens tumekamilisha usajili wake na wiki ijayo (Septemba 12, mwaka huu) atakuwa kikosini kujiunga na wachezaji wenzake kambini kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Makanya.

Aliongeza kuhusu kikosi hicho kitaenda kuweka wapi kambi, alieleza itaamuliwa hivi karibuni baada ya mabosi wa timu hiyo watakaporejea nchini wakitokea Malawi ambapo wako na timu kubwa (Simba) inakabiliwa na mechi ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Watakaporejea viongozi tutafahamu ni wapi tutaenda kuweka kambi pia tumejua tuko kundi gani na tunacheza na nani baada ya ratiba ya makundi kutoka leo (jana)," alisema meneja huyo.



Nahodha wa Timu ya Gofu ya Wanawake ya Taifa, Hawa Wanyeche akishusha bendera ya Tanzania ikiwa ni ishara ya kuhitimisha michuano ya mchezo huo ya Afrika iliyomalizika kwenye viwanja vya Gymkhana jijini, Dar es Salaam juzi. Tanzania ilimaliza katika nafasi ya tatu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yang'aka timu kuboronga

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Tanzania ikimaliza katika nafasi ya tatu katika mashindano ya gofu ya Afrika, serikali imewakumbusha wanamichezo kujituma na kuweka mbele uzalendo wanapopeperusha bendera ya nchi michuano mbalimbali ya kimataifa.

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, alisema hayo katika hafla ya kukabidhi zawadi kwa washindi wa mashindano ya gofu iliyofanyika kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere jijini, Dar es Salaam juzi.

Mchengerwa alisema, wizara yake itaanza kufuatilia timu zote za taifa zinazofanya vizuri na wale wasiofanya vyema kufundishwa yale ambayo Watanzania wanayataka.

"Nawaagiza viongozi mfanye tathmini ya timu zote za taifa za michezo yote ambazo hazifanyi vizuri katika michuano ya kimataifa na kuwapa siku 14 kutoa ripoti, ni bora kufanya uamuzi mgumu lakini wenye tija na manufaa kwa Watanzania," alisema Mchengerwa.

Waziri huyo alipongeza Timu ya Taifa ya Gofu ya Wanawake kwa kumaliza katika nafasi ya tatu pamoja na Twiga Stars ambayo ilitinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya COSAFA, yanayoendelea huko Afrika Kusini.

"Kwa kweli wanawake mmebadilisha taswira katika anga ya kimataifa, haya ni matunda ya Rais wetu Samia Suluhu Hassan, kwa kuwekeza kwenye sekta ya michezo," alisema waziri huyo.

Afrika Kusini ndio waliibuka mabingwa wa michuano hiyo ya Afrika ya gofu wakati Morocco wao walimaliza katika nafasi ya pili.

## Polisi Tanzania yang'ara majeshi

**Na Camila Bonanza, TUDARco**

TIMU ya mpira wa wavu ya Jeshi la Polisi Tanzania imeibuka na ushindi wa seti 3-1 dhidi ya wenzao wa Eswatini katika Michezo ya Majeshi inayoendelea kwenye Uwanja wa Ndani wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Tanzania, iliendelea kufanya vyema katika michezo hiyo baada ya kushika nafasi ya kwanza na ya pili kwenye mbio za nyika kwa upande wa wanawake katika umbali wa kilomita 10, zilizofanyika kwenye viwanja vya Chuo Kikuu (UDSM) huku nafasi ya tatu ikichukuliwa na Zimbabwe.

Katika soka Namibia walipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Msumbuji baada ya kupata bao la kwanza dakika ya 26 kupitia kwa Lina Katuta huku dakika ya 32, Steiza Sumbura akiisawazishia Msumbiji wakati Tweukondajela Amukoto akiifungia Namibia goli la ushindi dakika ya 56.

Katika upande wa wavu kwa wanawake, timu ya Jeshi la Polisi Tanzania iliwafunga wenzao wa Zimbabwe seti 3-2, katika mchezo uliokuwa na ushindani.

Hata hivyo, katika netiboli wenyeji Polisi Tanzania ilibanwa na Eswatini kwa kutoka sare ya mabao 30-30.

## Dodoma Jiji FC kumaliza uteja

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Dodoma Jiji ambayo haijaonja ladha ya ushindi tangu kuanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara imesema haitakubali kuona inapoteza mechi ijayo ya ligi hiyo baada ya kubaini mapungufu yaliyosababisha kupokea vichapo.

Dodoma Jiji itashuka ugenini kuwakabili Singida Big Stars, kesho kwenye Uwanja wa Liti mkoani Singida.

Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Masoud Djuma, alisema kiufundi tayari amerekebisha baadhi ya makosa na anaamini kesho watapambana kurejesha heshima ya timu yao kwa kupata ushindi.

"Dodoma Jiji ni timu kubwa, hatustahili kufungwa mechi tatu mfululizo, wachezaji wanatakiwa warudishe heshima yao kwa kushinda, kulikuwa na matatizo kadhaa ambayo tumeyarekebisha, nadhani sasa utakuwa ni mwanzo wa kufanya vyema," Djuma alisema.

Mrundi huyo alisema katika mechi mbili za mwanzo, pamoja mapumziko ya mechi za kimataifa, yamemfanya kupata kikosi cha kwanza pamoja na muunganiko wa timu, hivyo hana wasiwasi wa kupata pointi tatu katika mchezo wa kesho.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**BELLINGHAM ANUKIA LIVERPOOL**
KLABU ya Liverpool inapanga kumsajili kiungo wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19 ifikapo mwakani. ***(Bild - via Twitter)***

**FRANK AIKATAA BRIGHTON**
KOCHA wa Brentford, Thomas Frank amekanusha uvumi anawania nafasi iliyoachwa na Graham Potter katika kikosi cha Brighton, akisema "sijamaliza biashara "na "sina furaha sana" kuwa hapa. ***(Independent)***

**AUBAMEYANG ATANG'ARA**
CHELSEA ina uhakika usajili wa Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 33 ambaye alishitushwa na kufukuzwa kwa Thomas Tuchel, atang'ara chini ya kocha mpya wa Blues hao, Graham Potter. ***(Telegraph)***

**BAYERN YAMKANA KANE**
MKURUGENZI wa Soka wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic, amekanusha klabu hiyo kuhusishwa na mchakato wa kumsajili straika wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29, katika msimu ujao wa majira ya joto. ***(Talksport)***

**CHELSEA YAMTAJA AMORIM**
CHELSEA tayari inamfikiria Kocha Mkuu wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim, kama mrithi wa Graham Potter kama atashindwa kupata mafanikio na The Blues hao. ***(Daily Star)***

**KARIUS ANUKIA NEWCASTLE**
KLABU ya Newcastle United inakaribia kumsajili golikipa mwenye umri wa miaka 29 ambaye ni raia wa Ujerumani, Loris Karius, aliyeondoka Liverpool mapema mwaka huu. ***(Chronicle)***

**LLORIS AMHOFIA POGBA**
GOLIKIPA wa Tottenham Hotspur, Hugo Lloris, mwenye umri wa miaka 35 ana shaka kuhusu mchezaji mwenzake, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 29, kama atacheza Kombe la Dunia mwishoni mwa mwaka huu. ***(Football Italia)***

**HAG ALIMTAKA BROBBEY**
KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag alitaka kumfanya straika, Brian Brobbey mwenye umri wa miaka 20, kuwa usajili wake wa tatu wa kipindi cha majira ya joto baada ya kutua kwa Lisandro Martinez na Antony. ***(Sun)***

**MUDRYK KUTUA ARSENAL**
ARSENAL wanaweza kufufua nia ya kumsajili winga wa Shakhtar Donetsk na Timu ya Taifa ya Ukraine, Mykhaylo Mudryk mwenye umri wa miaka 21, wakati wa dirisha la Januari. ***(ESPN)***

**TUCHEL, TAJIRI KILIUMANA**
UHUSIANO mbaya kati ya Thomas Tuchel aliyefukuzwa Chelsea na mmiliki wa klabu hiyo, Todd Boehly ulianza wakati walipopishana kauli kuhusu kumsajili nyota wa Manchester United, Cristiano Ronaldo. ***(Metro)***

**COSTA, WOLVES KIMEELEWEKA**
KLABU ya Wolves jana ilitarajiwa kukamilisha usajiliwa, Diego Costa kwa uhamisho huru na kumpa mkataba wa mwaka mmoja mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea mwenye umri wa miaka 33. ***(Times)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GRIEZMANN SASA AKUBALI MATOKEO

Ni muda mchache wa kucheza alionao na kuinusuru Atletico kutozwa...

**MADRID, Hispania**

ANTOINE Griezmann amekubali ana kikomo cha kucheza kwa dakika 30 kwa mechi msimu huu kutokana na Atletico Madrid kutaka kukwepa kipengele ambacho kingewalazimu kuilipa Barcelona euro milioni 40.

Mfaransa huyo ametoka kwenye benchi takriban dakika 30 kabla ya kumalizika kwa kila mechi hadi sasa msimu huu, na hiyo si bahati mbaya.

Iwapo atacheza zaidi ya hapo, kifungu kingeanzishwa ambacho kitawalazimu Atletico Madrid kuilipa Barcelona, klabu yake mama euro milioni 40 ili kumsajili moja kwa moja.

Hawataki kufanya hivyo kwani atapatikana akiwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu.

Kutokana na hali hiyo, kuna uwezekano ataanzia benchi katika kila mechi hadi wakati huo.

"Ndivyo ilivyo, imetoka mikononi mwangu," alisema akiwaambia waandishi wa habari baada ya kufunga bao la ushindi dhidi ya Porto katika mechi yao ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, juzi.

"Nina mshukuru Mungu kwa kuwa hapa. Familia yangu ina furaha, bila shaka nataka zaidi, lakini nitatoa kila kitu nilicho nacho kwa dakika nilizo nazo.

"Ninahisi kama mtu wa klabu, nina furaha hapa na nataka tu kucheza hapa na kutoa kila kitu kwa ajili ya klabu."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,029,4
MECHI KALI
CADIZ CF
VERSUS
BARCELONA
1 | 10.08
X | 5.32
2 | 1.28
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa airtel money EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# MAWAKALA WAOGELEA FEDHA ULAYA

**NYON, Uswisi**

RIPOTI ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), inaonyesha mawakala wa soka walipata pauni milioni 430.8 katika dirisha la usajili wa majira ya joto lililofungwa mwanzoni mwa mwezi huu.

FIFA imetoa ripoti ya muhtasari inayoelezea uchambuzi wa shughuli za uhamisho wa kimataifa katika majira ya joto.

Imefichua mawakala wa soka kwa pamoja waliweka benki karibu asilimia 10 ya jumla ya thamani ya pauni bilioni 4.36 ya uhamisho wa wachezaji wa kiume.

Mwaka huu pia ulishuhudia idadi ya juu ya rekodi ya wachezaji wa kiume na wa kike waliohamishwa kote ulimwenguni.

Ripoti pia imeonyesha uwiano wa ada za huduma ya wakala kwa ada za uhamisho wakati wa dirisha la usajili la katikati ya mwaka umeongezeka kutoka asilimia 6.1 hadi asilimia 9.9 katika miaka 10 iliyopita.

Jumla ya thamani ya mwaka huu ya dirisha la uhamisho kwa wanaume ni pauni bilioni 4.36 inapita ya mwaka uliopita, ikiongezeka kwa asilimia 29.7.

Biashara nyingi za uhamisho wa majira ya joto zilifanywa katika soka la Uingereza, huku Ligi Kuu England ikitumia rekodi ya pauni bilioni 1.9.

Rekodi zaidi zilivunjwa, ambapo usajili wa Manchester United wa pauni milioni 81.3 wa Antony ukiwa uhamisho wa gharama kubwa zaidi wa siku ya mwisho wa Ligi Kuu England.

Ingawa siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili England ilikuwa Septemba Mosi, dirisha la uhamisho la nchi kadhaa za Ulaya kama vile Uturuki lilimalizika jana.

# Conte amwagia sifa Richarlison

**LONDON, England**

KOCHA Mkuu wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte, amemmwagia sifa Richarlison kwa kuendeleza ndoto yake ya kwanza kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Fowadi huyo wa Brazil alifunga mabao mawili pekee wakati Spurs ilipofungua kampeni ya Ulaya kwa ushindi wa magoli 2-0 nyumbani dhidi ya Marseille, Jumatano.

Richarlison hapo awali alizungumza kuhusu kujiunga na Tottenham ili kutimiza ndoto yake ya kucheza Ligi



ya Mabingwa Ulaya, na Conte anaamini alikuwa anastahili nafasi hiyo.

"Kwanza kabisa nina furaha kwa Richy kwa sababu alistahili kuwa na usiku kama huu," alisema Conte baada ya mechi.

"Nakumbuka sana tulipomsajili alisema 'Siwezi kusubiri kucheza na kusikiliza muziki wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.' Si maneno mengi bali ni maneno muhimu kwangu.

"Leo namkumbuka na kusema 'Richy nakumbuka ulichosema, usiku wa leo una nafasi. Furahia wakati huu na ujaribu kadri ya uwezo wako. Alijitahidi sana na kutusaidia kupata pointi tatu kwenye mchezo mgumu kwa sababu Marseille ni timu nzuri sana.

401,974/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/09/22 | 16:00 | AC Ajaccio vs Nice | 3.13 | 3.03 | 2.38 |
| 02. 11/09/22 | 16:00 | Angers vs Montpellier | 2.42 | 3.46 | 2.72 |
| 03. 11/09/22 | 16:00 | Toulouse vs Reims | 2.22 | 3.41 | 3.07 |
| 04. 11/09/22 | 16:00 | Bologna vs Fiorentina | 2.90 | 3.35 | 2.38 |
| 05. 11/09/22 | 16:00 | Lecce vs AC Monza Brianz | 2.24 | 3.34 | 3.14 |
| 06. 11/09/22 | 16:00 | Sassuolo vs Udinese | 2.64 | 3.43 | 2.54 |
| 07. 11/09/22 | 16:00 | Ilves Tampere vs Inter Turku | 2.83 | 3.33 | 2.43 |
| 08. 11/09/22 | 16:00 | Honka vs HJK Helsinki | 2.69 | 3.24 | 2.59 |
| 09. 11/09/22 | 16:30 | FC Koln vs Union Berlin | 2.38 | 3.31 | 2.87 |
| 10. 11/09/22 | 17:00 | Cercle Brugge vs Royal Antwerp | 2.84 | 3.44 | 2.37 |
| 11. 11/09/22 | 19:00 | Aalesunds vs Sarpsborg | 2.35 | 3.48 | 2.84 |
| 12. 11/09/22 | 19:00 | Ham-Kam vs Viking | 2.98 | 3.28 | 2.36 |
| 13. 11/09/22 | 20:00 | CS Maritimo vs Gil Vicente | 2.78 | 3.13 | 2.59 |
| 14. 11/09/22 | 20:00 | FC Arouca vs Boavista | 2.63 | 3.08 | 2.78 |
| 15. 11/09/22 | 20:00 | Kayserispor vs Antalyaspor | 2.59 | 3.34 | 2.64 |
| 16. 11/09/22 | 21:45 | Monaco vs Lyon | 2.46 | 3.46 | 2.67 |
| 17. 11/09/22 | 22:00 | Betis vs Villarreal | 2.79 | 3.38 | 2.44 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 10/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 3575 | Rayo Vallecano vs Valencia | 2.54 | 3.09 | 2.84 |
| 16:00 | 1542 | Moroka Swallows FC vs Stellenbosch | 2.55 | 2.75 | 3.10 |
| 16:00 | 1917 | Napoli vs Spezia | 1.23 | 5.97 | 9.76 |
| 16:00 | 2446 | Coastal Union vs Polisi Tanzania | 2.23 | 2.66 | 3.64 |
| 16:00 | 4664 | Kansanshi Dynamos vs Nkwazi | 2.36 | 2.56 | 3.50 |
| 16:00 | 5180 | Amazulu vs Chippa Utd | 1.94 | 2.91 | 4.51 |
| 16:30 | 1265 | Hoffenheim vs Mainz | 2.23 | 3.49 | 2.89 |
| 16:30 | 1279 | RB Leipzig vs Borussia Dortmund | 2.34 | 3.61 | 2.66 |
| 16:30 | 2128 | Eintracht Frankfurt vs VfL Wolfsburg | 2.02 | 3.50 | 3.35 |
| 16:30 | 4237 | Bayern Munchen vs Stuttgart | 1.14 | 7.82 | 13.03 |
| 16:30 | 5456 | Hertha BSC vs Bayer Leverkusen | 3.45 | 3.80 | 1.90 |
| 17:00 | 2428 | Kortrijk vs Mechelen | 2.57 | 3.47 | 2.52 |
| 17:00 | 2838 | Konyaspor vs Hatayspor | 1.72 | 3.76 | 4.42 |
| 17:15 | 3397 | Espanyol vs Sevilla FC | 2.83 | 3.14 | 2.51 |
| 17:30 | 2065 | CSKA Moscow vs FC Krasnodar | 1.64 | 3.80 | 4.81 |
| 17:30 | 4676 | Famalicao vs Benfica | 6.82 | 4.62 | 1.40 |
| 17:30 | 5953 | NEC Nijmegen vs Fortuna Sittard | 1.86 | 3.61 | 3.76 |
| 18:00 | 1654 | Josko Ried vs RB Salzburg | 9.87 | 5.72 | 1.21 |
| 18:00 | 5772 | Paris St Germain vs Brest | 1.11 | 8.33 | 19.98 |
| 18:30 | 2545 | Orlando Pirates vs TS Galaxy FC | 1.74 | 3.20 | 5.20 |
| 18:30 | 3312 | OFI Crete vs Panetolikos | 2.03 | 3.22 | 3.67 |
| 18:30 | 4268 | CS Constantine vs HB Chelghoum Laid | 1.41 | 4.03 | 7.08 |
| 18:45 | 2886 | ASO Chlef vs Paradou AC | 2.85 | 2.85 | 2.51 |
| 19:00 | 1782 | Inter vs Torino | 1.42 | 4.51 | 6.42 |
| 19:00 | 4226 | St. Gallen vs FC Sion | 1.73 | 3.87 | 4.22 |
| 19:15 | 2716 | RFC Seraing vs Brugge | 6.42 | 4.61 | 1.42 |
| 19:15 | 2808 | Oostende vs Eupen | 2.09 | 3.62 | 3.12 |
| 19:15 | 5812 | PAS Giannina vs Levadiakos | 1.99 | 3.22 | 3.82 |
| 19:30 | 1550 | Cadiz CF vs Barcelona | 10.08 | 5.32 | 1.28 |
| 19:30 | 3753 | Schalke 04 vs VfL Bochum | 2.02 | 3.50 | 3.35 |
| 19:45 | 4604 | Ajax vs Heerenveen | 1.17 | 7.01 | 12.01 |
| 19:45 | 5155 | Akhmat Grozny vs Nizhny Novgorod | 1.74 | 3.65 | 4.30 |
| 20:00 | 1245 | Fatih Karagumruk vs Giresunspor | 1.92 | 3.46 | 3.76 |
| 20:00 | 1986 | Sporting Lisbon vs Portimonense | 1.33 | 5.02 | 8.23 |
| 20:00 | 3613 | Odense vs Copenhagen | 4.52 | 3.77 | 1.70 |
| 20:00 | 4585 | Teplice vs Sparta Prague | 6.34 | 4.40 | 1.48 |
| 20:00 | 5493 | Apoel Nicosia vs Aris Limassol | 1.99 | 3.38 | 3.68 |
| 20:15 | 3385 | FC Ashdod vs Maccabi Tel Aviv | 6.50 | 4.33 | 1.40 |
| 21:00 | 4438 | Mamelodi Sundowns vs Golden Arrows | 1.62 | 3.60 | 5.40 |
| 21:30 | 1397 | Ionikos Nikea FC vs Atromitos | 2.25 | 3.12 | 3.22 |
| 21:30 | 3223 | U Craiova SA vs Rapid Bucuresti | 2.75 | 3.00 | 2.60 |
| 21:30 | 5598 | FC Winterthur vs FC Luzern | 2.86 | 3.46 | 2.30 |
| 21:45 | 2404 | Sampdoria vs AC Milan | 5.81 | 4.21 | 1.49 |
| 21:45 | 3750 | OH Leuven vs Charleroi | 2.75 | 3.60 | 2.30 |
| 22:00 | 1172 | Marseille vs Lille | 1.94 | 3.57 | 3.57 |
| 22:00 | 1537 | Atletico Madrid vs Celta Vigo | 1.62 | 3.74 | 5.45 |
| 22:00 | 2014 | SBV Excelsior vs Emmen | 3.06 | 3.41 | 2.18 |
| 22:00 | 2587 | US Biskra vs JS Saoura | 2.71 | 2.81 | 2.66 |
| 22:05 | 4823 | HNK Gorica vs Dinamo Zagreb | 5.51 | 4.14 | 1.48 |
| 22:30 | 1997 | Porto vs GD Chaves | 1.15 | 7.05 | 16.11 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# GEITA GOLD FC MATUMAINI KIBAO IKIWAVAA WASUDANI

**Na Saada Akida**

MATAJIRI wa madini, Geita Gold wanatarajia kurusha karata yao ya kwanza katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Hilal Alsahil ya Sudan Kaskazini itakayochezwa kesho jijini Khartoum.

Geita Gold FC ambao wamefadhiliwa na Kampuni ya Uchimbaji Madini Geita (GGML) waliweka kambi jijini Dar es Salaam kwa wanatarajiwa kurudiana na Wasudan hao siku nne baada ya mechi hiyo ya kwanza.

Hata hivyo, Geita Gold FC iliondoka nchini bila nyota wake wawili tegemeo, Saido Ntibazonkiza ambaye jina lake haliko katika orodha ya wachezaji waliosajiliwa kushiriki mashindano ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF) na mshambuliaji, George Mpole, ambaye ameugua ghafla.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Geita Gold FC, Fred Minziro, alisema wamejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo na anatambua utakuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa.


Minziro alisema kikosi chake kimekwenda kupambana kutafuta matokeo chanya na anaamini watatimiza malengo yao na kurejea nyumbani kumalizia kazi waliyoianza ugenini.

"Mechi itakuwa ngumu, nimepata nafasi ya kuona baadhi ya michezo ya wapinzani wetu, nimeona ubora na madhaifu yao, tumejiandaa kwa ajili ya kutafuta matokeo chanya katika mchezo wetu wa Jumapili," alisema Minziro.

Msemaji wa Geita Gold FC, Hemed Kivuyo alithibitisha, Ntibanzokiza na Mpole, hawakuondoka na timu hiyo kutokana na sababu mbalimbali.

"Tulifuata taratibu zote katika usajili, baada ya kushauriwa tumeamua kutosafiri naye, amebaki Dar es Salaam akiendelea kujifua, Mpole alikuwa katika msafara lakini ghafla alimfuata kocha (Minziro) na kumwambia anajisikia vibaya hawezi kusafiri," alisema Kivuyo.

Mpole ndiye mfungaji bora wa msimu uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambaye alikuwa akichuana na Fiston Mayele wa Yanga.



Wachezaji wa Geita Gold FC wakiwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere muda mfupi kabla ya kuanza safari ya kuelekea Sudan kuwavaa wenyeji wao Hilal Alsahil katika mechi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa kesho nchini humo . **PICHA: MTANDAO**

# KMKM, Tripoli kibaruani Afrika

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MABAHARIA wa KMKM wanatarajia kuikaribisha Al Ahli Tripoli kutoka Libya katika mchezo wa kwanza wa hatua ya awali wa mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa leo kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Amaan, Visiwani hapa.

Kocha Mkuu wa KMKM, Hemedi Morocco, aliliambia gazeti hili wamejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo na wamejipanga kuondoka na matokeo bora. Morocco alisema wataingia katika mechi hiyo kwa tahadhari na kamwe hawataki kuona wanaanza michuano hiyo kwa kupoteza.

"Maandalizi yote yamekamilika, tunajua mechi itakuwa ngumu na yenye ushindani, tumejiandaa kukabiliana na hali hiyo, tumedhamiria kuanza kwa ushindi," alisema Morocco ambaye anasaidiwa na Ame Msimu.

Kocha huyo pia amewaomba mashabiki mbalimbali wa soka Zanzibar kujitokeza kwa wingi kuishangilia timu yao ili kuhakikisha inapata ushindi na inasonga mbele katika michuano hiyo.

Wawakilishi wengine wa Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ni Kipanga ambao kesho watavaana na Hial FC ya Sudan Kusini katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

# Michezo

Jumamosi Septemba 10, 2022
Nipashe



## Griezmann sasa akubali matokeo



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Nelson Okwa (kushoto) na kiungo, Peter Banda wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji Nyasa Big Bullets itakayochezwa leo jijini Lilongwe, Malawi. **PICHA: SIMBA SC**

## Twiga Stars yachapwa

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), imekubali kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Zambia (She- Polopolo), katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya COSAFA iliyochezwa mjini Port Elizabeth jana mchana.

Kwa matokeo hayo, Twiga Stars imevuliwa ubingwa wa michuano hiyo na sasa itasubiri kucheza mchezo wa kuwania nafasi ya tatu.

Timu hizo zilikwenda mapumziko zikiwa sare ya bao 1-1, lakini kipindi cha pili kilipoanza, ushindani ulionekana kutawala kutoka katika pande zote mbili.

Mabao ya She Polopolo katika mchezo huo yalifungwa na Barbara Banda na Chisha Misozi huku Margareth Belemu akijifunga na kuipa Twiga Stars bao pekee katika mechi hiyo.

"Tumefungwa na timu bora, lakini tukiweka pembeni matokeo, tumeondoka na faida kubwa, nilidhamiria kutumia mashindano haya kama sehemu ya kuiandaa Serengeti Girls kuelekea fainali za Kombe la Dunia," Bakari Shime, Kocha Mkuu wa Twiga Stars, alisema jana baada ya mechi hiyo.

# Simba, Yanga mguu sawa Afrika

## ●●●Nabi, Mgunda kila mmoja aahidi kuanza kwa kicheko katika michuano ya Ligi ya Mabingwa...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa, Simba na Yanga zote za jijini, Dar es Salaam zikiwa kwenye viwanja tofauti, leo zinatarajiwa kuanza kampeni ya kuwania taji la michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Yanga itaanza kampeni zake kwa kucheza dhidi ya mabingwa wa Ligi Kuu Sudan, Zalan FC inayotumia Uwanja wa Benjamin Mkapa wakati Simba yenyewe itakuwa jijini Lilongwe nchini Malawi kuwakabili wenyeji Nyasa Big Bullets.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, alisema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya mechi hiyo ambayo anatarajia itakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu ya ubora waliokuwa nao wapinzani wao.

Nabi alisema anaimani wachezaji wake watafanya vizuri katika mchezo huo wa ugenini lakini wakitumia uwanja ambao wamezoea na kupata matokeo chanya.

"Tumejiandaa vizuri na tunawaheshimu wapinzani wetu kwa sababu nao wamejiandaa kwa ajili ya kutafuta matokeo chanya, ninaimani utakuwa mchezo mgumu na ushindani mkubwa.

"Yale madhaifu yaliyojitikeza tumefanyia kazi na kuendelea kuwakumbusha wachezaji wetu kuhakikisha tunacheza kwa nidhamu ya hali ya juu, hasa kwenye safu ya ulinzi kutokana na uimara wa ubora wa safu ya ushambuliaji ya wapinzani wetu," alisema Nabi.

Mtunisia huyo alisema kucheza mchezo huo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ni faida kwao ambapo watajiwekea mazingira mazuri kuelekea mechi ya marudiano kwa kupambana na kushinda michezo yote miwili.

Aliongeza alisema malengo yake ni kufika hatua ya makundi na ili kufikia huko watacheza kwa tahadhari na vile vile kuwaheshimu Wasudani hao.

Zalan itashuka katika mechi hiyo ikiwa na kocha mpya, Baping Alliab, ambaye ametua klabuni hapo Agosti 18, mwaka huu akitokea Al Hilal Wau ya Sudan Kusini na kuchukua mikoba iliyoachwa na Richard Ola.

Mshindi wa jumla katika mechi hiyo atakutana na mshindi kati ya St. George ya Ethiopia au Al Hilal ya Sudan.

Wekundu wa Msimbazi wenyewe leo saa 9:00 mchana sawa na saa 10:00 jioni hapa Tanzania itawavaa Nyasa Big Bullets kwenye Uwanja wa Bingu Mutharika uliokо Lilongwe.

Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, aliliambia gazeti hili amekiandaa vyema kikosi chake na anaamini vijana watafuata maelekezo aliyowapa ili kuhakikisha wanapata ushindi na kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele.

"Yalikuwa ni mazoezi ya kwanza kwangu kwenye timu hii na baada ya hapo nilikaa na kuzungumza nao, siku zote ubora wa kazi ya mwalimu unatokana na kujituma kwa wachezaji, tunaweza kufundisha na kuzungumza yote, lakini kama utayari hakuna ni kazi bure, nashukuru wameelewa, wamenisikiliza na hata jinsi walivyopokea mazoezi, unaona kabisa kuna kitu wanataka kufanya, kwa hiyo tupo tayari na mechi, tuna matumaini ya kufanya vizuri," alisema Mgunda.

Aliongeza amewaona wapinzani wao, na hivyo amekiandaa kikosi chake kuwakabili na hatimaye kuvuna kile wanachokihitaji katika mechi hiyo ya kwanza ya hatua ya awali.

"Nimewaona wapinzani wetu, nimeangalia baadhi ya video zao, ni timu ambayo sio ya kubeza, wanacheza kitimu na wanacheza nyumbani, tahadhari zote tutachukua," alisema Mgunda.

Katika hatua nyingine, mabosi wa Simba wamewaondoa hofu mashabiki wao kuhusiana na elimu aliyonayo Mgunda kuelekea mechi hiyo kama taratibu na kanuni za Shirikisho la Soka Afrika (CAF) zinavyohitaji.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kila kitu kimekamilika, ikiwamo kuwasili kwa kikosi kazi na mashabiki waliofika kuwashangilia.

"Tuna mashabiki wa Simba ambao ni Watanzania walioko nchini Malawi, lakini kuna mashabiki ambao waliwasili hapa kwa ajili ya kuishangilia na kuwapa nguvu wachezaji, vijana hawatokuwa wapweke," alisema Ahmed.

Mshindi wa jumla wa mechi hiyo atakutana na kati ya Red Arrows ya Zambia au Primeiro de Agosto ya Angola.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >